AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: +251 115 517 700 Fax: +251 115 517 844
Website: www.au.int

**BARAZA KUU**
**Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Tano**
**Tarehe 18-19 Julai 2024**
**Accra, GHANA**

**EX.CL/Dec.1265 - 1278(XLV)**
Lugha chanzi: Kiingereza

# MAAMUZI

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI NDOGO ZA KAMATI YA WAWAKILISHI WA KUDUMU (PRC)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** mapendekezo ya PRC kuhusu ripoti za Kamati zake Ndogo, kwa kuzingatia maoni yaliyotolewana Nchi Wanachama.

## I. KUHUSU KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI NDOGO YA USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA NA WATAALAM WA KIUFUNDI WA KAMATI YA MAWAZIRI WA FEDHA KUMI NA WATANO (F-15) - Doc: EX.CL/1518(XLV)

**Baraza Kuu,**

### BAJETI YA UMOJA WA AFRIKA KWA MWAKA 2025

**Baraza Kuu,**

2. **LINAZINGATIA** Ripoti za PRC na Mkutano wa Pamoja wa Kamati Ndogo za Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala, Programu na Mikutano na Wataalamu wa Kiufundi wa F-15;

3. **LIKITAMBUA** changamoto ya mazingira ya kiuchumi duniani ambayo yalilazimisha kupitishwa kwa hatua kali za kubana matumizi kwa bajeti ya 2025, na kwa kuzingatia viwango vya utekelezaji vya miaka iliyopita, na majadiliano ya Mkutano wa Pamoja**, LINAAMUA** kuwekea kikomo michango iliyotathminiwa ya Nchi Wanachama katika Bajeti ya AU ya 2025 kwa dola za Marekani 200,000,000.

4. **LINAIDHINISHA** Bajeti ya jumla ya AU ya mwaka 2025 ya **dola za Marekani 608,248,546** iliyogawanywa kama ifuatavyo:

   A. Bajeti ya Kawaida ya **dola za Marekani 555,319,415** iliyogawanywa kama ifuatavyo:

   i) Bajeti ya Uendeshaji ya **dola za Marekani 167,045,485** itakayofadhiliwa kama ifuatavyo:

   - Dola za Marekani 163,371,481 (98%) zilizotathminiwa kwa Nchi Wanachama,
   - Dola za Marekani 3,674,004 (2%) kutoka mfuko wa Matengenezo;

ii) Bajeti ya Programu ya **dola za Marekani 388,273,929** itakayofadhiliwa kama ifuatavyo[1]:

a) Nchi Wanachama, Taasisi za Kiafrika na Vyanzo vya Ndani (dola za Marekani 87,520,383) – 22.5%, inajumuisha:

- Dola za Marekani 36,628,518 (9.4%) kutokana kwenye tathmini ya Nchi Wanachama;
- Dola za Marekani 500,000 (0.1%) kutoka Mfuko wa Matengenezo;
- Dola za Marekani 1,318,199 (0.3%) kutoka Mfuko wa Utawala;
- Dola za Marekani 1,774,367 (0.5%) kutoka riba ya Mfuko wa Amani;
- Dola za Marekani 46,664,299 (12.0%) kutoka Taasisi za Afrika; ambayo inajumuisha dola za Marekani 1,687,278 za Msaada wa Kiufundi.
- Dola za Marekani 635,000 (0.2%) kutoka Michango ya Hiari ya Nchi Wanachama.

b) Dola za Marekani 300,753,546 (77.5%) kutoka kwa Wabia wa Kimataifa, ambazo zinajumuisha dola za Marekani 63,239,895 za Msaada wa Kiufundi.

B. Operesheni za Kuleta Amani zenye bajeti ya **dola za Marekani 52,929,131,** zinazofadhiliwa na Wabia wa Kimataifa;

C. Kwa ujumla, bajeti ya AU ya 2025 itafadhiliwa kama ifuatavyo:

| Ugawaji wa Fedha | Uendeshaji | Programu | PSO | Jumla | % Mgao |
|---|---|---|---|---|---|
| Mchango uliotathminiwa wa Nchi Wanachama | 163,371,481 | 36,628,518 | - | **200,000,000** | **32.9%** |
| Mfuko wa Matengenezo | 3,674,004 | 500,000 | | **4,174,004** | **0.7%** |
| Mfuko wa Usimamizi/Mapato Yaliyozalishwa | | 1,318,199 | | **1,318,199** | **0.2%** |
| Mfuko wa Amani (Riba) | | 1,774,367 | | **1,774,367** | **0.3%** |
| Taasisi za Kiafrika | | 46,664,299 | | **46,664,299** | **7.7%** |
| Michango ya Hiari ya Nchi Wanachama | | 635,000 | | **635,000** | **0.1%** |
| Wabia wa Kimataifa | | 300,753,546 | 52,929,131 | **353,682,677** | **58.1%** |
| **Jumla ya Bajeti 2025** | **167,045,485** | **388,273,929** | **52,929,131** | **608,248,546** | **100%** |

Jedwali 1: vyanzo vya fedha vya bajeti ya 2025

22. [1]Wajumbe wa Ufalme wa Morocco uliingia kwenye bajeti ya programu ya OSC na katika masuala ya bajeti yanayoshughulikia Kikosi cha Dharura cha Afrika.

| Vyombo | Mchango uliotathminiwa wa Nchi Wanachama | | | Mfuko wa Matengenezo | | | Mfuko wa Usimamizi/Mapato Yaliyozalishwa | Mfuko wa Amani (Riba) | Taasisi za Kiafrika | Mchango wa Hiari wa Nchi Wanachama | Wabia wa Kimataifa | Jumla ya Bajeti 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Bajeti ya Uendeshaji | Programu | Jumla ya Tathmini | Bajeti ya Uendeshaji | Programu | Jumla | Programu | Programu | Programu | Programu | Programu | Uendeshaji | Programu | Jumla |
| AUC | 92,381,586 | 11,608,876 | **103,990,462** | 2,325,231 | 500,000 | **2,825,231** | 537,133 | 1,774,367 | 6,732,608 | - | 140,035,736 | 94,706,816 | 161,188,720 | **255,895,536** |
| PAP | 9,501,416 | 309,152 | **9,810,568** | 77,000 | - | **77,000** | - | - | - | - | 462,649 | 9,578,416 | 771,800 | **10,350,216** |
| AFCHR (Mahakama) | 7,934,629 | 2,551,983 | **10,486,612** | 34,000 | - | **34,000** | - | - | - | - | 67,614 | 7,968,629 | 2,619,597 | **10,588,226** |
| ACHPR (Tume) | 4,256,753 | 685,889 | **4,942,642** | 20,025 | - | **20,025** | - | - | - | - | - | 4,276,778 | 685,889 | **4,962,667** |
| ECOSSOC | 1,923,079 | 427,477 | **2,350,556** | 73,850 | - | **73,850** | - | - | - | - | - | 1,996,929 | 427,477 | **2,424,406** |
| AUDA-NEPAD | 9,980,059 | 6,098,873 | **16,078,932** | 372,884 | - | **372,884** | 431,426 | - | 7,000,740 | - | 64,560,782 | 10,352,944 | 78,091,820 | **88,444,764** |
| AUCIL | 241,207 | 139,156 | **380,363** | - | - | **-** | - | - | - | - | - | 241,207 | 139,156 | **380,363** |
| Bodi ya Ushauri kuhusu Rushwa | 1,541,164 | 169,844 | **1,711,008** | 8,714 | - | **8,714** | - | - | - | - | - | 1,549,878 | 169,844 | **1,719,722** |
| Baraza la Amani na Usalama | - | 1,782,979 | **1,782,979** | - | - | **-** | - | - | - | - | - | - | 1,782,979 | **1,782,979** |
| ACERWC | 1,374,993 | 203,240 | **1,578,233** | 3,600 | - | **3,600** | - | - | - | - | 293,874 | 1,378,593 | 497,114 | **1,875,707** |
| APRM | 5,501,965 | 749,937 | **6,251,902** | 58,125 | - | **58,125** | - | - | 239,307 | - | 2,638,097 | 5,560,091 | 3,627,341 | **9,187,431** |
| **OFISI MAALUM** | | | | | | | | | | | | | | |
| AFREC | 1,416,895 | 87,317 | **1,504,212** | 25,825 | - | **25,825** | - | - | - | - | 2,762,635 | 1,442,720 | 2,849,952 | **4,292,672** |
| IPED | 698,192 | 24,408 | **722,600** | 19,500 | - | **19,500** | - | - | - | - | - | 717,692 | 24,408 | **742,100** |
| CIEFFA | 616,821 | 25,000 | **641,821** | 16,300 | - | **16,300** | - | - | - | - | 326,445 | 633,121 | 351,445 | **984,566** |
| PAU | 2,644,924 | 6,780,609 | **9,425,533** | 60,000 | - | **60,000** | - | - | - | 635,000 | 4,201,925 | 2,704,924 | 11,617,534 | **14,322,458** |
| AIR | 675,903 | 78,424 | **754,327** | 9,950 | - | **9,950** | - | - | - | - | - | 685,853 | 78,424 | **764,277** |
| AfCDC | 4,943,853 | 2,330,688 | **7,274,541** | 18,000 | - | **18,000** | - | - | 27,191,456 | - | 54,157,540 | 4,961,853 | 83,679,684 | **88,641,537** |
| AOSTI | 367,454 | 25,892 | **393,346** | 17,490 | - | **17,490** | - | - | - | - | - | 384,944 | 25,892 | **410,836** |
| AFRIPOL | 1,037,080 | 50,000 | **1,087,080** | 62,420 | - | **62,420** | - | - | - | - | 877,366 | 1,099,500 | 927,366 | **2,026,866** |
| BARAZA LA MICHEZO | 739,881 | - | **739,881** | 11,000 | - | **11,000** | 349,640 | - | - | - | 151,000 | 750,880 | 500,640 | **1,251,520** |
| ASRIC | 155,680 | 115,200 | **270,880** | - | - | **-** | - | - | - | - | - | 155,680 | 115,200 | **270,880** |
| AfCFTA | 7,280,900 | 615,693 | **7,896,594** | 142,590 | - | **142,590** | - | - | 5,500,188 | - | 20,318,953 | 7,423,490 | 26,434,834 | **33,858,324** |
| PANASTAT | 204,769 | - | **204,769** | 3,500 | - | **3,500** | - | - | - | - | - | 208,269 | - | **208,269** |

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| STATAFRIC | 1,328,536 | 52,500 | **1,381,036** | 6,000 | - | **6,000** | - | - | - | - | 3,539,940 | 1,334,536 | 3,592,440 | **4,926,976** |
| ACSRM- Mali | 549,880 | 52,486 | **602,366** | 48,400 | - | **48,400** | - | - | - | - | - | 598,280 | 52,486 | **650,766** |
| Mwangalizi – Morocco | 526,527 | 241,461 | **767,989** | 30,000 | - | **30,000** | - | - | - | - | - | 556,527 | 241,461 | **797,989** |
| COC – Khartoum | 562,108 | 24,675 | **586,783** | 37,000 | - | **37,000** | - | - | - | - | - | 599,108 | 24,675 | **623,783** |
| PCRD | 817,943 | 32,000 | **849,943** | 41,000 | - | **41,000** | - | - | - | - | 468,000 | 858,943 | 500,000 | **1,358,943** |
| ACBF | - | 105,000 | **105,000** | - | - | **-** | - | - | - | - | 1,143,066 | - | 1,248,066 | **1,248,066** |
| ACSRT | 2,057,289 | 43,336 | **2,100,625** | 25,200 | - | **25,200** | - | - | - | - | 144,129 | 2,082,489 | 187,465 | **2,269,954** |
| CELHTO | 1,185,918 | 45,292 | **1,231,210** | 71,700 | - | **71,700** | - | - | - | - | - | 1,257,618 | 45,292 | **1,302,910** |
| ACALAN | 766,809 | 50,502 | **817,311** | 54,700 | - | **54,700** | - | - | - | - | - | 821,509 | 50,502 | **872,011** |
| *AU Continental Logistics Base* | 157,265 | 1,011,050 | **1,168,315** | - | - | **-** | - | - | - | - | 475,802 | 157,265 | 1,486,852 | **1,644,117** |
| *African Med. Agency* | - | 29,400 | **29,400** | - | - | **-** | - | - | - | - | 949,771 | - | 979,171 | **979,171** |
| AfSA | - | 28,300 | **28,300** | - | - | **-** | - | - | - | - | 3,178,223 | - | 3,206,523 | **3,206,523** |
| Shirika la Kibinadamu la Afrika | - | 51,880 | **51,880** | - | - | **-** | - | - | - | - | - | - | 51,880 | **51,880** |
| **JUMLA kabla ya PSOs** | **163,371,481** | **36,628,518** | **200,000,000** | **3,674,004** | **500,000** | **4,174,004** | **1,318,199** | **1,774,367** | **46,664,299** | **635,000** | **300,753,546** | **167,045,485** | **388,273,929** | **555,319,415** |
| **SHUGHULI ZA KULETA AMANI** | | | | | | | | | | | | | | |
| Kikosi Kazi cha Pamoja cha Kimataifa (MNJTF) | - | - | **-** | | | - | | - | | | 19,106,382 | - | 19,106,382 | **19,106,382** |
| POST ATMIS[2] | - | - | | | | | | | | | 23,822,749 | - | 23,822,749 | **23,822,749** |
| Mbinu ya Mwitikio wa Mapema (ERM) | - | - | | | | | | | | | 10,000,000 | - | 10,000,000 | **10,000,000** |
| **Jumla ya Msaada wa Amani** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **-** | **52,929,131** | **-** | **52,929,131** | **52,929,131** |
| **JUMLA** | **163,371,481** | **36,628,518** | **200,000,000** | **3,674,004** | **500,000** | **4,174,004** | **1,318,199** | **1,774,367** | **46,664,299** | **635,000** | **353,682,677** | **167,045,485** | **441,203,060** | **608,248,546** |

Jedwali la 2: Bajeti iliyounganishwa ya 2025 kwa Chombo, Taasisi na Ofisi[3]

[2] Kiasi hiki ni cha muda kwa ajili ya Shughuli za kuleta amani za AU nchini Somalia huku yakisubiriwa mahitimisho na maamuzi ya wazi juu ya nini cha kufanya baada ya Ujumbe wa ATMIS yatakayofanywa na Chombo husika, ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Ufadhili.
[3] Kiasi cha dola za Marekani 609,577 hakijatengwa na kimewekwa kwenye Bajeti ya Uendeshaji ya AUC kwa ajili ya mgao wa Kiprogramu.

5. **LINAZINGATIA** mchanganuo wa bajeti ya 2025 kulingana na kitengo cha gharama na kwa Mashirika/Afisi Maalum kama ifuatavyo:

| Vyombo | Gharama ya Wafanyakazi | Matumizi ya Uendeshaji | Matumizi ya mtaji | Jumla ya Uendeshaji | Programu | Jumla 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| AUC | 74,823,137 | 19,237,639 | 646,040 | **94,706,816** | 161,188,720 | **255,895,536** |
| PAP | 7,682,572 | 1,834,844 | 61,000 | **9,578,416** | 771,800 | **10,350,216** |
| AFCHR (Mahakama) | 7,215,915 | 752,714 | - | **7,968,629** | 2,619,597 | **10,588,226** |
| ACHPR (Tume) | 3,410,321 | 866,458 | - | **4,276,778** | 685,889 | **4,962,667** |
| ECOSSOC | 1,788,167 | 208,762 | - | **1,996,929** | 427,477 | **2,424,406** |
| AUDA-NEPAD | 9,317,259 | 951,685 | 84,000 | **10,352,944** | 78,091,820 | **88,444,764** |
| AUCIL | - | 241,207 | - | **241,207** | 139,156 | **380,363** |
| Bodi ya Ushauri kuhusu Rushwa | 934,075 | 615,803 | - | **1,549,878** | 169,844 | **1,719,722** |
| Baraza la Amani na Usalama | - | - | - | **-** | 1,782,979 | **1,782,979** |
| ACERWC | 1,111,525 | 267,069 | - | **1,378,593** | 497,114 | **1,875,707** |
| APRM | 4,651,382 | 859,614 | 49,095 | **5,560,091** | 3,627,341 | **9,187,431** |
| **OFISI MAALUM** | | | | | | |
| AFREC | 1,311,614 | 111,281 | 19,825 | **1,442,720** | 2,849,952 | **4,292,672** |
| IPED | 581,159 | 130,534 | 6,000 | **717,692** | 24,408 | **742,100** |
| CIEFFA | 480,253 | 152,868 | - | **633,121** | 351,445 | **984,566** |
| PAU | 2,072,765 | 632,158 | - | **2,704,924** | 11,617,534 | **14,322,458** |
| AIR | 652,255 | 33,597 | - | **685,853** | 78,424 | **764,277** |
| AfCDC | 4,399,731 | 562,122 | - | **4,961,853** | 83,679,684 | **88,641,537** |
| AOSTI | 357,939 | 19,155 | 7,850 | **384,944** | 25,892 | **410,836** |
| AFRIPOL | 877,864 | 199,816 | 21,820 | **1,099,500** | 927,366 | **2,026,866** |
| BARAZA LA MICHEZO | 641,571 | 109,309 | - | **750,880** | 500,640 | **1,251,520** |
| ASRIC | - | 155,680 | - | **155,680** | 115,200 | **270,880** |
| AfCFTA | 6,780,766 | 642,724 | - | **7,423,490** | 26,434,834 | **33,858,324** |
| PANASTAT | 170,809 | 37,461 | - | **208,269** | - | **208,269** |
| STATAFRIC | 1,151,399 | 183,138 | - | **1,334,536** | 3,592,440 | **4,926,976** |
| Mwangalizi - Mali | 488,067 | 76,213 | 34,000 | **598,280** | 52,486 | **650,766** |
| Mwangalizi - Morocco | 481,677 | 74,851 | - | **556,527** | 241,461 | **797,989** |
| Mwangalizi - Khartoum | 486,847 | 78,261 | 34,000 | **599,108** | 24,675 | **623,783** |
| PCRD | 757,813 | 68,130 | 33,000 | **858,943** | 500,000 | **1,358,943** |
| ACBF | - | - | - | **-** | 1,248,066 | **1,248,066** |
| ACSRT | 1,988,767 | 92,522 | 1,200 | **2,082,489** | 187,465 | **2,269,954** |
| CELHTO | 1,014,314 | 177,304 | 66,000 | **1,257,618** | 45,292 | **1,302,910** |
| ACALAN | 630,042 | 191,468 | - | **821,509** | 50,502 | **872,011** |
| *AU Continental Logistics Base* | 157,265 | - | - | **157,265** | 1,486,852 | **1,644,117** |
| *African Med. Agency* | - | - | - | **-** | 979,171 | **979,171** |
| AfSA | - | - | - | **-** | 3,206,523 | **3,206,523** |
| Shirika la Kibinadamu la Afrika | - | - | - | **-** | 51,880 | **51,880** |
| *PSOs* | | | | **-** | 52,929,131 | **52,929,131** |
| **JUMLA kabla ya PSOs** | **136,417,269** | **29,564,385** | **1,063,831** | **167,045,485** | **441,203,060** | **608,248,546** |

Jedwali la 3: Bajeti ya 2025 kulingana na kundi la matumizi kwa kila Chombo, Taasisi na Ofisi

6. **PIA LINAZINGATIA** bajeti iliyosambazwa kama ifuatavyo:

| Na. | Kwa Aina ya Bajeti | Bajeti | % Mgao |
|---|---|---|---|
| 1 | Bajeti Kuu | 257,060,100 | **42%** |
| 2 | *Fedha zinazopita kwa mashirika mbalimbali (Pass Through Funds)* | 58,906,909 | **10%** |
| 3 | Msaada wa Kiufundi | 64,927,173 | **11%** |
| 4 | Mradi Maalum | 7,379,748 | **1%** |
| 5 | Msaada wa Amani | 52,929,131 | **9%** |
| 6 | Uendeshaji | 167,045,485 | **27%** |
| | | **608,248,546** | **100%** |

Jedwali la 4: Bajeti ya 2025 kulingana na aina ya kundi

7. **LINATAMBUA** kiasi cha **dola za Marekani 19,004,582** kilichojumuishwa katika Bajeti ya Programu ya AU ya 2025, ambazo zilithibitishwa hapo awali, na linaidhinisha kiasi hicho kwa misingi ya kipekee.

8. **LINAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1189(XLII), ulioiagiza Kamisheni kuunda Mfumo wa Usimamizi wa Mtiririko wa Fedha unaounganisha ugawaji wa fedha na mipango ya idara ya robo mwaka kwa kuzingatia ukubwa wa shughuli na programu, kama ilivyoainishwa katika Uamuzi EX.CL/Dec.1143(XL) aya ya 18 (IV), na kutoa fedha kwa wakati ili kuwezesha idara mbalimbali kutekeleza programu kama ilivyopangwa. **LINASISITIZA** haja ya Kamisheni kuandaa mpango wa kina wa usimamizi wa mtiririko wa fedha unaolenga kuelekeza fedha kwa wakati na kwa ufanisi kwa programu zilizopangwa, na hivyo kuwezesha upangaji na utekelezaji wa shughuli na programu.

9. **LINASISITIZA** haja ya Kamisheni ya kutekeleza uamuzi EX.CL/Dec.1168(XLI) aya ya 82 ya Julai 2022, uliopitishwa mjini Lusaka, Zambia, ambao uliiagiza Kamisheni kuunda Kikundi Kazi kinachojumuisha Nchi Wanachama, Wataalamu wa Kiufundi wa F-15, AUDA-NEPAD, Kurugenzi ya Fedha ya Kamisheni, Ofisi ya Mipango Mikakati na Utekelezaji (OSPD), Ofisi (*Bureau*) ya Makamu Mwenyekiti, Ofisi ya Mshauri wa Sheria na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, ili kushughulikia mwingiliano na urudufu kati ya Vyombo, Wakala na Idara za AU.

10. **LIKITAMBUA** shabaha za Johannesburg, **LINAIAGIZA** Kamisheni kufanya upembuzi yakinifu kuhusu pendekezo la kulipa sehemu ya michango iliyotathminiwa katika fedha za kitaifa kulingana na Kanuni za Fedha za AU.

11. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuzipa Nchi Wanachama, ifikapo Februari 2025, orodha ya kina ya wafanyakazi wote wanaofanya kazi katika Umoja wa Afrika ambao

wanafadhiliwa na wabia wa kimataifa. Orodha hii inapaswa kujumuisha mchanganuo wa utaifa wao, na taasisi ambazo wanafanyia kazi.

12. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuandaa mkakati wa kina wa kukusanya rasilimali unaolenga kupata na kusimamia ipasavyo ufadhili kutoka kwa wabia wa kimataifa kwa namna ya kuwajibika na endelevu huku ikihakikisha kuwa fedha zilizokusanywa zinawiana na vipaumbele vya Umoja wa Afrika.

13. **LINAIAGIZA** Kamisheni kutumia uwezo wa ndani wa tafiti na ripoti, kwa lengo la **kuboresha** ugawaji wa bajeti ya uendeshaji huku ikihakikisha utekelezaji mzuri wa programu.

14. **LINAZINGATIA** haja ya kupanga bajeti kwa ajili ya ushiriki wa Umoja wa Afrika katika shughuli za G20 kwa mwaka 2025 kwa kufuata utaratibu unaostahili na kwa kuzingatia haja ya kupokea wasilisho kamili kutoka kwa Kamisheni. **LINAAMUA** kwamba bajeti itajadiliwa wakati wa mkutano maalum ujao wa Baraza Kuu, uliopangwa kufanyika baadaye mwaka 2024.

## II. KUHUSU KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI NDOGO YA USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA WA MAMBO YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA (GSCBFAM) NA WATAALAM WA KIUFUNDI WA F-15

**Baraza Kuu,**

15. **LINAZINGATIA** Ripoti za PRC na Kikao cha Pamoja cha Kamati Ndogo za Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala na Wataalamu wa Kiufundi wa F-15.

16. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec .1233(XLIV) ambapo Kamisheni na Wataalamu wa Kiufundi wa F-15 waliagizwa kukamilisha kazi ya Sera ya Hazina na Uwekezaji, pamoja na Vigezo vya Uchaguzi wa Benki na kuiwasilisha kwa kuzingatiwa na PRC kupitia Kamati yake Ndogo inayohusika, **LINAPONGEZA** juhudi zilizofanywa kuhusiana na suala hili, na **LINAMUAGIZA** Mwenyekiti wa AUC kuidhinisha waraka wa Sera.

17. **LINAREJEA** Maamuzi ya Baraza Kuu EX.CL/ Dec.1218 (XLIII) na Ex.CL/Dec.1233(XLIV) kuhusu uundaji wa Sera ya Gharama ya Utawala Isiyo ya Moja kwa Moja ya AU, **LINAZINGATIA** juhudi zilizofanywa kuhusiana na hili na **LINAMUAGIZA** Mwenyekiti wa AUC kuidhinisha waraka wa Sera.

18. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1240(XLIV), ambapo Kamisheni iliombwa kukamilisha Mbinu za Matumizi na Michango ya Mfuko wa Amani na kuwasilisha ripoti kwa **Halmashauri** Kuu. **LINAZINGATIA** hatua iliyofikiwa hadi sasa na **KUIOMBA** Kamisheni kuwasilisha ripoti ya mwisho ya Kikao cha Kawaida cha 46 cha Baraza Kuu mwezi Februari 2025.

**19.** **LINAREJEA ZAIDI** Uamuzi EX.CL/Dec.1240(XLIV) wa mwezi Februari 2024, ambao UNASISITIZA kwamba ufadhili wowote wa baadae, ikiwa ni pamoja na ukomo wa CFR ya 2025 na Miradi ya Majaribio, lazima ufuate mchakato unaofaa kupitia Kikao cha Pamoja cha Kamati ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Jumla wa Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala na Kamati ya Kiufundi ya Wataalam wa F15 Experts (F15) na ufadhili huo utategemea utendaji na malengo yaliyofikiwa katika ufadhili uliotangulia kwa taasisi hizi kwa kuzingatia Sheria za Fedha za AU, Ibara ya 21 ya Mkataba unaohusu Kuanzisha Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika nan a chombo kilichoidhinishwa kinachohusiana na Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika.

**Uamuzi kuhusu bajeti ya ziada kwa 2024**

**20.** **LINAKUMBUSHIA** Uamuzi AU/Dec.866(XXXVII), ambapo Mkutano ulimteua Rais William Ruto wa Kenya kuwa Mhamasishaji mpya wa AU kuhusu Marekebisho ya Kitaasisi, pamoja na Uamuzi AU/Dec.873(XXXVII), ambalo liliiomba Kamisheni kujumuisha bajeti ya ushiriki wa Umoja wa Afrika katika mikutano ya G-20.

**21.** **LINAIDHINISHA** bajeti ya ziada kiasi cha **US$2,903,715** kwa mwaka 2024 kama ilivyoainishwa hapa chini.

i) **USD 1,023,159** kwa ajili ya ushiriki wa Umoja wa Afrika katika mikutano ya G-20 kutoka kwenye Mfuko wa Akiba.
ii) **USD 1,097,000** kwa ajili ya Idara ya Afya, Masuala ya Kiutu na Maendeleo ya Jamii kupitia mchango wa hiari kutoka Afrika Kusini
iii) **USD 783,556** kwa ajili ya Kitengo cha Maboresho kutokana na michango ya Washirika

**22.** **LINAIDHINISHA** kwa namna ya kipekee, bila kuzingatia taratibu zilizopitia, kujumuishwa kwa bajeti iliyotajwa kwenye bajeti ya AU ya mwaka 2024.

**23.** **LINAIPONGEZA** Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kwa mchango wa hiari wa **USD 1,097,000** zilizotolewa kwa Kamisheni kwa ajili ya misaada ya kiutu katika eneo la Sahel

**24.** **LINAZINGATIA** pendekezo la Kamisheni la kuundwa kwa Kitengo cha Uratibu wa G20, na kusisitiza umuhimu wa kufuata utaratibu unaostahili katika suala hilo kupitia Kamati Ndogo husika za PRC.

**25.** **LINAOMBA** kwamba PRC ifahamishwe mara kwa mara na Kamisheni kuhusu maendeleo yaliyopatikana kuhusiana na mchakato wa mageuzi.

## III. KUHUSU MKUTANO WA PAMOJA WA KAMATI NDOGO ZA KAMATI YA WAWAKILISHI WA KUDUMU (PRC) KUHUSU USIMAMIZI NA URATIBU WA JUMLA JUU YA MASUALA YA BAJETI, FEDHA NA UTAWALA (GSCBFAM), MAGEUZI YA KIMUUNDO NA WATAALAM WA KIUFUNDI WA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA WATANO WA FEDHA (F15) - EX.CL/1520(XLV)

**Baraza Kuu,**

**26.** **LINAREJEA** Ibara ya 9(2) ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika (Constitutive Act), ambayo inatoa mamlaka kwa Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi na Serikali kukasimu mamlaka na majukumu yake yoyote yale kwa Chombo chochote cha Umoja wa Afrika.

**27.** **LINAREJEA ZAIDI** Uamuzi wa Mkutano Mkuu 891 (XXXVIII) wa Februari 2024 aya ya 2 ambapo Mkutano Mkuu "UNAAMUA" kukasimu mamlaka yake kwa Baraza Kuu kujadili na kupitisha, wakati wa Mkutano wake wa 45 mwezi Juni/Julai 2024, miundo ya:

- Shirika la Kibinadamu la Afrika (AfHA) na ;
- Kituo cha Ubora cha Masoko Jumuishi cha Afrika (AIMEC).

**Kuhusu Muundo wa Shirika la Kibinadamu la Afrika (AfHA)**

**28.** **LINAZINGATIA** muundo na bajeti pendekezwa iliyowasilishwa na Kamisheni;

**29.** **LINAPITISHA** Muundo wa nafasi 55 kama inavyoorodheshwa kwenye jedwali A hapa chini na bajeti ya utekelezaji wa awamu ya 1 (nafasi 12) ya Shirika la Kibinadamu la Afrika kwa mwaka 2025 ya kiasi cha dola za Marekani 924,175.94;

**30.** **LINASISITIZA** haja ya kufanya michakato yote ya kuajiri kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Wafanyakazi na Mfumo wa idadi ya kikomo (*quota system*) wa Umoja wa Afrika. Mchakato wa kuajiri unapaswa kufanywa kwa awamu kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

**A. Nafasi zilizoidhinishwa za Shirika la Kibinadamu la Afrika zimeorodheshwa katika jedwali hapa chini pamoja na awamu ya utekelezaji inayotumika:**

| Divisheni / Kitengo | Jina la Kazi | Daraja | Awamu ya Utekelezaji | Idadi ya nafasi |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Executive Secretary* | (D1)[4] | 2025 | 1 |

[4]Daraja la D1 lililopewa Katibu Mtendaji litashikiliwa kwa muda mfupi ikisubiriwa kukamilika kwa mchakato wa usanifishaji wa uainishaji na upangaji madaraja wa nafasi zote za kawaida za AU, ikiwa ni pamoja na Wakuu wa taasisi za AU (tazama aya ya 14 ya uamuzi huu).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Senior Gender Officer* | P3 | itaamuliwa | 1 |
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Senior Legal Officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Senior Communication Officer* | P3 | itaamuliwa | 1 |
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Secretary* | GSA5 | 2025 | 1 |
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Driver* | GSB7 | 2025 | 1 |
| Ofisi ya Katibu Mtendaji | *Administrative Assistant / clerk* | GSA 5 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Principal Officer, Finance and Administration* | P4 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Senior Finance officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Finance Officer* | P2 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Senior ICT Officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Assistant ICT* | GSA5 | itaamuliwa | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Senior HR officer* | P3 | itaamuliwa | 1 |
| Kitengo cha Fedha, Utumishi na Utawala | *HR officer* | P2 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Senior Admin Officer* | P3 | itaamuliwa | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Admin assistant* | GSA5 | itaamuliwa | 1 |
| Kitengo cha Fedha, HR, na Utawala | *Drivers / Mail Runner* | GSB7 | itaamuliwa | 3 |
| Kitengo cha dharura na mwitikio wa kibinadamu | *Principal Officer, Emergency and humanitarian response* | P4 | 2025 | 1 |
| Kitengo cha dharura na mwitikio wa kibinadamu | *Senior Officer, Emergency, and humanitarian response* | P3 | itaamuliwa | 2 |
| Vituo na Bohari za Kanda | *Principal Officer Regional Centre Coordination* | P4 | itaamuliwa | 5 |
| Vituo na Bohari za Kanda | *Senior Officers Regional centres (North, South, West, central and East)* | P3 | itaamuliwa | 10 |
| Vituo na Bohari za Kanda | *National Finance and administrative officers (N,* | P2 | itaamuliwa | 5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | *S, W, C, E)* | | | |
| Vituo na Bohari za Kanda | *Driver / Mail Runner (N, S, W, C, E)* | GSB7 | itaamuliwa | 5 |
| Kitengo cha urekebishaji na ustahimilivu (*Adaptation and resilience building unit*) | *Principal Officer, Adaptation, and resilience building* | P4 | itaamuliwa | 1 |
| Kitengo cha urekebishaji na ustahimilivu | *Senior Officer, Adaptation, and resilience building* | P3 | itaamuliwa | 2 |
| Ubia, ukusanyaji wa rasilimali na kujenga uwezo | *Principal Officer, Partnership and Resource mobilization* | P4 | 2025 | 1 |
| Ubia, ukusanyaji wa rasilimali na kujenga uwezo | *Senior Partnership and resource mobilization officer* | P3 | itaamuliwa | 1 |
| Onyo la mapema la kibinadamu na kuzuia shida (*Humanitarian early warning and crisis prevention*) | *Principal Officer, Humanitarian early warning, and crisis prevention* | P4 | itaamuliwa | 1 |
| Onyo la mapema la kibinadamu na kuzuia shida | *Senior Officers, Humanitarian early warning, and crisis prevention* | P3 | itaamuliwa | 2 |
| **Jumla ya idadi ya nafasi kwenye muundo** | | | | **55** |

*TBD - itaamuliwa, kulingana na aya ya 7 ya uamuzi huu.*

**31.** **LINAELEZA** wasiwasi juu ya jinsi Kamisheni inavyoshughulikia takwimu za muundo wa Shirika la Kibinadamu la Afrika;

**32.** **LINAIELEKEZA** F-15 kuchunguza pendekezo la Kamisheni la Utekelezaji wa Shirika la Kibinadamu la Afrika lenye ukomo wa jumla ya nafasi 55 kwa awamu mbalimbali, na kutoa ripoti kwenye Mkutano wa Pamoja wa Kamati Ndogo za Usimamizi na Uratibu wa Jumla kuhusu Masuala ya Bajeti, Fedha na Utawala na Mageuzi ya Kimuundo, kwa ajili ya kuwasilishwa baadae kwa Mkutano Mkuu ili kujadiliwa mnamo Februari 2025, kupitia PRC na Baraza Kuu;

**33.** **LINAAMUA** kwamba utekelezaji wa uamuzi huu utategemea kupatikana kwa fedha.

**Kuhusu Muundo wa Kituo cha Ubora cha Masoko Jumuishi cha Afrika (AIMEC)**

**34.** **LINAZINGATIA** muundo na bajeti iliyopendekezwa ya Kituo cha Ubora cha Masoko Jumuishi cha Afrika;

**35.** **LINAPITISHA** muundo wa Kituo cha Ubora cha Masoko Jumuishi cha Afrika **chenye** nafasi 27 kama zinavyoorodheshwa kwenye jedwali B hapa chini na bajeti ya utekelezaji wa awamu ya 1 (2025) na awamu ya 2 (2026);

### B. Nafasi zilizoidhinishwa za Kituo cha Ubora cha Masoko Jumuishi cha Afrika zinaorodheshwa katika jedwali hapa chini pamoja na awamu ya utekelezaji inayotumika:

| Divisheni/Kitengo | Jina la kazi | Daraja | Awamu ya Utekelezaji | Idadi ya nafasi |
|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji | *Executive Director* | D1 | 2025 | 1 |
| Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji | *Senior Legal Officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji | *Principal Senior Officer* | P4 | 2026 | 1 |
| Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji | *Secretary* | GSA4 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji (*Division of Operations*) | *Head of Operations Division* | P5 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Senior Finance Officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Senior Human Resources Officer* | P3 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Procurement Officer* | P2 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Information and Technology Officer* | P2 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Marketing and Communication Officer* | P2 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Protocol Officer* | P2 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Security Supervisor* | GSA5 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Accountant Assistant* | GSA5 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Clerk* | GSA4 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Messenger* | GSB5 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Driver* | GSB5 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Uendeshaji | *Driver* | GSB5 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Utafiti, Uvumbuzi, Maendeleo ya Miradi na Ufadhili | *Head of Division Research, Innovation, Project Development and Funding)* | P5 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Utafiti, Uvumbuzi, Maendeleo ya Miradi na Ufadhili | *Senior Monitoring and Evaluation Officer* | P3 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Utafiti, Uvumbuzi, Maendeleo ya Miradi na Ufadhili | *Senior Project and Innovation Analyst* | P3 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Utafiti, Uvumbuzi, Maendeleo | *Database and Programme Officer* | P2 | 2026 | 1 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ya Miradi na Ufadhili | | | | |
| Divisheni ya Utafiti, Uvumbuzi, Maendeleo ya Miradi na Ufadhili | *Administrative Assistant* | GSA5 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati na Utetezi wa Sera | *Head of Division Partnership and Strategic Engagement and Policy Advocacy* | P5 | 2025 | 1 |
| Divisheni ya Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati na Utetezi wa Sera | *Senior Policy Officer on Partnership and Strategic Engagement* | P3 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati na Utetezi wa Sera | *Senior Policy Officer on Policy Advocacy* | P3 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati na Utetezi wa Sera | *Grant Officer* | P3 | 2026 | 1 |
| Divisheni ya Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati na Utetezi wa Sera | *Administrative Assistant* | GSA5 | 2026 | 1 |
| **Jumla ya idadi ya nafasi kwenye Muundo** | | | | **27** |

36. **LINAAMUA** kuwa utekelezaji wa uamuzi huu utategemea upatikanaji wa fedha;

37. **LINASISITIZA** haja ya kufanya michakato yote ya kuajiri kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Wafanyakazi na Mfumo wa idadi ya kikomo (*quota system*) wa Umoja wa Afrika. Mchakato wa kuajiri unapaswa kufanywa kwa awamu kama ifuatavyo:

### C. Ajira ya Awamu na gharama ya wafanyakazi iliyoidhinishwa

| Awamu | Jumla ya idadi ya Wafanyakazi | | Jumla ya gharama |
|---|---|---|---|
| | Ajira mpya | Jumla | |
| Awamu ya 1: 2025 | 13 | 13 | 1,022,699 |
| Awamu ya 2: 2026 | 14 | 27 | 1,765,072 |
| **Jumla** | **27** | **27** | **2,787,771** |

**Kuhusu masuala yaliyoibuka wakati wa kujadili miundo hii miwili:**

38. **LINAZINGATIA** hali ya sintofahamu iliyopo kutokana na kukosekana kwa vigezo vinavyoeleweka kuhusu utoaji wa majina na madaraja ya Wakuu wa taasisi za AU**;**

**39.** **LINAIAGIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuandaa pendekezo la mchakato wa kina wa kusanifisha utoaji madaraja wa nafasi zote za AU, ikiwa ni pamoja na Wakuu wa taasisi za AU, na kutoa ripoti kwa Vyombo vya Sera vya AU ifikapo Februari 2025;

**40.** **LINASISITIZA** kwamba uendeshaji mzuri wa mashirika yote mapya ya Umoja wa Afrika unapaswa kutekelezwa katika muktadha wa mchakato mpana wa mageuzi ya kitaasisi wa AU utakaokamilika ifikapo Februari 2025.

**Kuhusu Ukaguzi wa Ujuzi na Tathmini ya Umahiri (SACA)**

**41.** **LINAREJEA** Uamuzi wa Baraza Kuu Dec.1218 (XLIII) wa Julai 2023 aya ya 38 ambapo Baraza Kuu "LINAIOMBA" Bodi ya Wakaguzi wa Nje (BoEA) ya AU kufanya ukaguzi wa kina kuhusu mchakato wa SACA na kutoa ripoti kwenye mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu mnamo Februari 2024.

**42.** **LINAREJEA ZAIDI** Uamuzi wa Baraza Kuu Dec. 1233(XLIV) wa Februari 2024 aya ya 86 ambapo Baraza Kuu "LINAIAGIZA" PRC, kupitia Kamati zake Ndogo husika, kwa kushirikiana kwa karibu na Kamisheni kuendelea kujadili ripoti za mchakato wa SACA, ikiwa ni pamoja na ripoti ya ukaguzi ya Bodi ya Wakaguzi wa Nje (BoEA) kuhusu SACA, na kuharakisha maendeleo ya suala hilo na kutoa ripoti kwenye Mkutano ujao wa Kawaida wa Baraza Kuu mnamo Julai 2024. **LINAAMUA** kufanya Mkutano Maalum kwa njia ya mtandao wa Baraza Kuu mnamo Oktoba 2024 ili kujadili ripoti ya maendeleo kuhusu utekelezaji wa mchakato wa SACA, bajeti kwa ajili ya shughuli za ushiriki wa AU kwenye G20, na kuhusu masuala yanayohusiana na masuala ya ukaguzi.

**Kuhusu Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko Afrika**

**43.** **LINAZINGATIA** maendeleo yaliyopatikana katika uendeshaji wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko, na haja ya kuhakikisha kuwa imethibitishwa kisheria na Ofisi ya Mshauri wa Sheria kabla ya kujadiliwa, na linaiagiza PRC kujadili pendekezo lililosasishwa baada ya kuthibitishwa kwake kisheria, na kuwasilisha ripoti yake kwa ajili ya kujadiliwa kwa Mkutano wa Kawaida wa 46 wa Baraza Kuu mnamo Februari 2025;

**44.** **LINAAGIZA ZAIDI** kwamba iwapo kuna ombi lolote la dharura la ufadhili, Africa CDC kupitia Kamisheni inapaswa kuwasilisha ombi kwa PRC, kwa mujibu wa mchakato unaofaa, kwa msingi wa kesi kwa kesi hadi kukamilika kwa pendekezo hilo mnamo Februari 2025.

## IV. KUHUSU KAMATI NDOGO YA MASUALA YA UKAGUZI – EX.CL/1522(XLV)

**Baraza Kuu,**

**45.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Ukaguzi na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo.

**KUHUSU RIPOTI YA SHUGHULI ZA OIO KWA MWAKA 2023**

**46.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Shughuli za OIO ya Mwaka 2023 na **LINAELEKEZA** yafuatayo:

(i) Ripoti za OIO zinapaswa kujumuisha kiasi kilichohifadhiwa kutokana na uchunguzi, pamoja na kiasi kinachopaswa kurudishwa na chombo na kuhakikisha ripoti za shughuli zinakuwa wazi zaidi na zinajumuisha zaidi maelezo juu ya mashirika na idara ambazo hazizingatii mapendekezo ya ukaguzi.

(ii) Mapendekezo ya ukaguzi wa OIO yanafaa kuelekezwa kwa uongozi wa Kamisheni au Mashirika kadri inavyofaa, ili maamuzi yaweze kufanyika.

(iii) Kamisheni ya kuhakikisha mfumo thabiti wa vikwazo unawekwa kwa wasimamizi wanaoshindwa kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi kulingana na maagizo ya Baraza Kuu.

A. <u>KUHUSU RIPOTI YA BoEA KUHUSU UKAGUZI WA KINA JUU YA SERA ZA MANUNUZI ZA AU, MICHAKATO YA MALIPO NA MASURUFU YOTE YALIYOSALIA KWA WASAMBAZAJI.</u>

**47.** **LINAZINGATIA** Ripoti na **KUIELEKEZA** Kamisheni kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi wa BOEA yaliyomo.

**48.** **LINAAGIZA ZAIDI** kama ifuatavyo:

(i) Kitengo cha Ununuzi cha AUC kinapaswa kutuma barua pepe pamoja na Ujumbe kwa Nchi Wanachama kuhusu Mpango wa Ununuzi na shughuli za ununuzi kwenye tovuti za AU, ili kuhusisha miji mikuu mbalimbali kwa ajili ya ushiriki mpana wa wasambazaji katika ofa za zabuni za Kamisheni.

(ii) Kamisheni kuweka vikwazo dhidi ya maafisa wanaokiuka mwongozo na kanuni za manunuzi. Kamisheni ya kuimarisha uratibu katika ngazi ya idara ili kuwezesha michakato ya manunuzi.

(iii) Kamisheni kutoa mchanganuo wa matumizi ya manunuzi inayoonyesha mgawanyo wake duniani ili kuwa na takwimu za kiasi kinachotumika katika Bara.

(iv) Ripoti ya manunuzi kujumuisha tathmini ya utendakazi kwa wasimamizi ili kuhakikisha uwajibikaji.

(v) Kamisheni kuhalalisha hali ya kiutawala ya wafanyakazi wanaohusika na manunuzi na kuepuka kutumia wafanyakazi wa muda mfupi.

(vi) Kamisheni kufuatilia malipo yaliyofanyika kwa wasambazaji bila kupelekwa, ikiwa ni pamoja na dola za Marekani 30,000 zilizolipwa kwa

Maziwisa Consultancy. Kamisheni kuwaorodhesha wafanyikazi wa Ushauri wa Maziwisa ilibainika kuhusishwa na malipo ya awali ya $30,000.

(vii) Kamisheni kuharakisha mapitio ya mwongozo wa manunuzi. Inapaswa kutumika kirahisi na kuondoa sura ambazo hazina umuhimu.

(viii) Kamisheni kuimarisha mfumo wa SAP kwa kuboresha ufasaha wa watumiaji. Kitengo cha Ununuzi kinapaswa kuufahamu zaidi mfumo wa SAP ili kuepuka matokeo ya ukaguzi yasiyo ya lazima.

(ix) Kamisheni inapaswa kuthibitisha mara kwa mara maingizo ya data katika mifumo ya SAP na AMERT pamoja na ucheleweshaji wa ununuzi unahitaji uhakiki wa mara kwa mara ili kuepuka makosa na ucheleweshaji katika utekelezaji wa matumizi.

(x) Wakurugenzi wanapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutekeleza matumizi ya mwongozo wa manunuzi.

(xi) Kamisheni kuweka ukomo wa muda katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kuepuka kuendeleza masuala ambayo hayajashughulikiwa na kujirudia kwa matokeo.

(xii) Kamisheni kutoa ripoti kwa Kamati Ndogo ya Ukaguzi mnamo Desemba 2024 kuhusu ufuatiliaji wa magari matatu (03) yaliyonunuliwa kutoka kwa Kampuni ya MACOM Trading PLC tangu Desemba 21, 2021 ambayo hayajapelekwa Somalia kwa zaidi ya miezi 22 sasa.

(xiii) Kamisheni kuhakikisha kuwa ina wasambazaji mbalimbali wa magari kwa ajili ya shughuli za kusaidia kuleta amani na kulinda amani.

B. <u>KUHUSU RIPOTI YA BoEA JUU YA UCHUNGUZI KUHUSU HALI YA KIASI CHOTE AMBACHO HAKIJAREJESHWA CHA MISHAHARA NA MASURUFU YALIYOLIPWA KWA WAFANYAKAZI, PAMOJA NA MASURUFU NA MIKOPO, NA KUFAA KWA TARATIBU ZA HATUA ZAIDI ZA KINIDHAMU, PALE INAPOFAA</u>

**49.** **LINAZINGATIA** Ripoti na **LINAIELEKEZA** Kamisheni kutekeleza mapendekezo yote ya ukaguzi yaliyomo.

**50.** **LINAAGIZA ZAIDI** kama ifuatavyo:

(i) OLC ihakikishe kwamba Amri za Mahakama zimeanzishwa kwa mikopo na malipo yote ya muda mrefu ambayo hayajalipwa ili kuyarejesha kwa usaidizi wa Nchi Wanachama na Interpol.

(ii) Kamisheni kuweka kikomo cha mikopo na malipo ya awali ya wafanyakazi na kuepuka mikopo mingi kwa afisa yule yule.

(iii) Kamisheni hakikishe kwamba wafanyakazi wote wanaoshindwa kulipa mikopo yao au mikopo yao imewekwa kwenye orodha nyeusi na hawapewi tena mikopo.

(iv) Kamisheni kuhakikisha kwamba mikopo yote na malipo ya awali yanaambatana na dhamana yenye uwezo wa kulipia mkopo mzima endapo mkopo huo haurejeshwa ndani ya muda uliowekwa.

(v) Kamisheni inapaswa kuhakikisha kwamba kwa mikopo yote ya Magari ina hadi urejeshaji wa mwisho wa mkopo uliowekwa na ofisa hati ya usajili wa gari.
(vi) Kamisheni kuweka adhabu kwa kutofuata siku 7 za kazi zilizowekwa kwa ajili ya ulipaji wa mikopo ya usafiri na Masurufu.

**C. <u>KUHUSU RIPOTI YA BoEA KUHUSU UKAGUZI WA KINA IKIJUMUISHA REKODI ZA WAFANYAKAZI AMBAZO HAZIKUSHUGHULIKIWA NA PwC NA PIA IKIJUMUISHA KIPINDI CHA 2019 HADI 2020 AMBACHO HAKIJASHUGHULIKIWA NA PwC KWENYE MAENEO YOTE YA UKAGUZI YANAYOTAKIWA</u>**

**51.** **LINAZINGATIA** Ripoti na **KUIELEKEZA** Kamisheni kutekeleza mapendekezo yote ya ukaguzi yaliyomo ndani yake.

**52.** **LINAELEKEZA ZAIDI** kamisheni:

(i) Kuwasilisha ripoti ambayo inayoeleza kwa kina matokeo na mapendekezo yote katika ripoti ya BoEA inayoonyesha yale ambayo tayari yametekelezwa na yale ambayo yanasubiriwa kueleza hatua za kurekebisha zilizochukuliwa na mpango wa utekelezaji unaoeleza hatua zilizochukuliwa pia mapendekezo ambayo hayajakamilika na muda wa kuyatekeleza ili kuboresha mchakato wa kuajiri hasa kuhusu uundaji wa Majopo, ufanisi wa taratibu na uzingatiaji wao wa Sheria na Kanuni za Wafanyakazi.
(ii) Kuhakikisha kwamba mpango wa kuajiri unaoonesha nafasi zitakazojazwa unapatikana miezi sita mapema ili kuwezesha Nchi Wanachama kuongeza uelewa kwa raia wao kwa ajili ya kuwasilisha maombi.
(iii) Kubuni utaratibu wa kuripoti mara kwa mara ili kuzifahamisha Nchi Wanachama kuhusu hatua ya michakato yote ya kuajiri, na maelezo ya changamoto zozote zilizojitokeza katika mchakato.
(iv) kusambaza mawasiliano ya kidiplomasia (*note verbale)* kwa Nchi Wanachama ili zipate picha ya matumizi yao ya idadi ya kikomo. Hii itahakikisha uwazi na uaminifu katika mchakato wa kuajiri.
(v) Kuweka utaratibu wa kinidhamu na vikwazo kwa wafanyakazi wanaohudumu katika jopo mbalimbali na wanaokiuka sera na taratibu za uajiri wa SRR na AU.
(vi) Kufanya uchunguzi wa Nchi Wanachama zenye uwakilishi mdogo katika robo ya tatu ya 2024 ili kubaini sababu za msingi za uhaba wa maombi na kupata suluhisho la kweli la matatizo.
(vii) Kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba wagombea ambao hawakufanikiwa ambao maombi yao yamekataliwa wanajulishwa moja kwa moja sababu za kwa nini maombi hayo yamekataliwa.
(viii) Kuweka utaratibu utakaoruhusu waombaji kuambatisha vyeti vyao wakati wa kutuma maombi yao ya awali.

(ix) Kuweka muundo wa rufaa wa kushughulikia malalamiko kutoka kwa wagombea kufuatia matokeo ya uteuzi wa wagombea na jopo la kuajiri.

**D. KUJADILI RIPOTI ZA OIO KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA VYOMBO MWAKA 2023**

**53.** **LINAZINGATIA** ripoti na **KUELEKEZA** Vyombo vyote vya AU kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ya OIO yaliyomo ndani yake.

**KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA AUC MWAKA 2023**

**54.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

(i) OIO inapaswa kufikiria upya matumizi ya neno "Inayoridhisha" katika ripoti zake na kutoa maelezo zaidi kuhusu changamoto nyingi za usimamizi zinazokabili mashirika mbalimbali. Pia inapaswa kuhakikisha kwamba mapendekezo yake yana muda ulio wazi wa utekelezaji.

(ii) Mipango ya kupunguza askari kwa askari wa ATMIS inapaswa kutekelezwa kulingana na maamuzi ya Mashirika ya Sera ya AU.

(iii) Idara za AUC zinapaswa kuboresha upangaji wao ili kuhakikisha utekelezaji bora wa kiufundi.

(iv) Vikwazo vinapaswa kuwekwa kwa idara ambazo hazitumii AMERT, pamoja na zile zinazotumia fedha za washirika kwa shughuli zisizohusiana na zile ambazo hazitoi majibu ya ripoti za ukaguzi. Vikwazo vinaweza kujumuisha kuzuia bajeti zilizotengwa za idara.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA AFRIKA CDC YA MWAKA 2023**

**55.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

(i) Menejimenti ya Afrika-CDC inapaswa kuonyesha uwazi zaidi katika utunzaji wa Fedha za Ziada kwa kuhakikisha kwamba Mchakato wa Bajeti wa Muungano unazingatiwa kikamilifu kwenye Fedha zao zote za Nje.

(ii) Uongozi wa Afrika-CDC unapaswa kuweka utaratibu wa kuhakikisha udhibiti ufaao wa Fedha za Ziada na pia kutoa ufikiaji wa gharama za ziada zinazotumiwa na Afrika-CDC kwa Wakaguzi wa AU. Mashauriano na OLC yafanyike kwa kutumia vipengele vipya au haja ya kupitia makubaliano ya ubia/MOU pale itakapolazimika.

(iii) AUC inapaswa kufanya ukaguzi wa kina maalum wa Fedha za Ziada za Afrika-CDC kwa kipindi cha kuanzia 2019-2024 na kutoa ripoti kwa Kamati Ndogo ya Masuala ya Ukaguzi.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA AfCHPR (MAHAKAMA) YA MWAKA 2023**

**56.** **LINAIAGIZA** AfCHPR:

(i) Kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti yake ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti kwa mwaka wa 2023.
(ii) Kuakisi malipo yaliyoidhinishwa katika Ripoti zao za Fedha.
(iii) Kuzingatia kikamilifu sheria za AU kabla ya kuamua kutumia rasilimali za Umoja wa Afrika.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA AUDA-NEPAD YA MWAKA 2023**

(i) AUDA-NEPAD inapaswa kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti ya mwaka 2023.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA PAP YA MWAKA 2023**

**57.** **LINAIAGIZA** PAP:

(i) Kuhakikisha kuwa michango yote kutoka kwa wabia iwe ya fedha taslimu au ya vitu, inahesabiwa na kuwekwa wazi katika rekodi zake, kulingana na matakwa ya IPSAS.
(ii) Kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti ya mwaka 2023.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA ACHPR (TUME) MWAKA 2023**

**58.** **LINAIAGIZA** ACHPR kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA AfCFTA YA MWAKA 2023**

**59.** **LINAIAGIZA** AfCFTA:

(i) Kufanya maombi ya fedha za ziada za dola za Marekani milioni 2.9 zilizoidhinishwa tangu mwaka 2022 na Baraza Kuu ili kuajiri (kupanda) wafanyakazi wanaohitajika ili kutimiza majukumu yake.
(ii) Kuweka mifumo ifaayo ya mipango na ufuatiliaji ili kuepuka utekelezaji mbovu wa kiufundi wa shughuli zake za programu.
(iii) Kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2023.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA APRM YA MWAKA 2023**

**60.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

(i) APRM inapaswa kutekeleza mapendekezo yote ya ukaguzi katika ripoti ya ukaguzi wa ndani kuhusu utekelezaji wa bajeti na kwa mwaka 2023.
(ii) Mashirika yote ya AU yanayoshindwa kufuata sera na taratibu za Kuendeleza Bajeti yanapaswa kukabiliana na matokeo.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA ECOSOCC YA MWAKA 2023**

**61.** **LINAIAGIZA** ECOSOCC kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti kwa mwaka wa 2023.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA AUABC YA MWAKA 2023**

**62.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

i) AUABC kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti yake ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti kwa mwaka wa 2023.
ii) AUABC kuhakikisha wanatengeneza bajeti halisi kwenye shughuli na programu zao kulingana na uwezo wa kutekeleza.
iii) Mchakato wa kuajiri Afisa Mwandamizi wa Sera unapaswa kuharakishwa na kukamilishwa ipasavyo.
iv) Haja ya kuhakikisha kuna uhusiano mzuri wa kazi na mawasiliano bora kati ya Sekretarieti na Bodi kwa lengo la kukamilishana na kufikia mamlaka ya AUABC.
v) OLC kuharakisha utafiti ulioombwa juu ya uwazi wa majukumu kati ya Sekretarieti na Bodi (yaani AUABC) kwa ajili ya mazingira bora ya kazi.

**KUHUSU UTENDAJI WA BAJETI YA ACERWC YA MWAKA 2023**

**63.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

i) ACERWC kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye Ripoti yake ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Utendaji wa Bajeti kwa mwaka wa 2023.
ii) Mchakato wa kuajiri wafanyikazi wakuu unapaswa kuharakishwa na kukamilishwa ipasavyo.

**KUHUSU RIPOTI ZA UTENDAJI WA JUMLA WA BAJETI YA MWAKA 2023**

**64.** **LINAAGIZA** kama ifuatavyo:

i) Kamisheni ya AU inapaswa kutoa mafunzo ya mara kwa mara (kwa robo mwaka) na kujenga uwezo kwa vyombo vyote vya AU hususan kwa wale wafanyakazi wanaotumia AMERT na SAP.

ii) Vyombo vyote vya AU vinapaswa kutumia kikamilifu matumizi ya AMERT na SAP katika kuripoti, ambapo kwa kushindwa kufanya hivyo vikwazo vinavyofaa vinapaswa kutumika.

iii) Vyombo vyote vya AU vinapaswa kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyomo kwenye ripoti za ukaguzi wa ndani kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023.

**KUHUSU KUCHAPISHWA KWA RIPOTI ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA ZA VYOMBO VYA UMOJA WA AFRIKA ZA MWAKA 2023**

**65.** **LINAIOMBA** PRC kujadili na kuidhinisha uchapishaji wa ripoti za Fedha Zilizokaguliwa za 2023 za mashirika ya AU kwa kuzingatia sheria za fedha za AU. Kujadiliwa kwa ripoti hizi zilizokaguliwa utafanywa baada ya Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka huko mnamo Julai 2024 mjini Accra.

## V. KUHUSU KAMATI NDOGO YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI JUNI 2024 – Doc.EX.CL/1523(XLV)A

**Baraza Kuu,**

### A. Ushirikiano wa AU na EU

**66.** **LINAIOMBA PRC,** kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Umoja wa Ulaya, kuendelea na mashauriano ili kuafikiana juu ya tarehe inayofaa ya kufanyika kwa Mkutano wa tatu wa Mawaziri wa AU na EU na Mkutano wa kwanza wa Kamati ya Ufuatiliaji utakaofanyika 2024, huko Brussels, Ubelgiji.

**67.** **LINAIOMBA ZAIDI** PRC, kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Umoja wa Ulaya, kuendelea kushirikisha wadau ili kukamilisha hati za matokeo ya Mkutano wa tatu (3) wa Mawaziri wa AU na EU na Mkutano wa kwanza wa Kamati ya Ufuatiliaji ya AU na EU.

### B. Ushirikiano wa Afrika na Uturuki

**68.** **LINAOMBA** kwamba Nchi Mwenyeji wa Mkutano wa Tatu wa Mapitio ya Mawaziri wa Afrika na Uturuki ichaguliwe kulingana na Ripoti ya Ujumbe wa Tathmini kufuatia kuzingatiwa nakupitishwa na PRC;

**69.** **LINAIOMBA** PRC kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni, nchi mwenyeji iliyotambuliwa na Türkiye **KUKUBALIANA** kuhusu tarehe mahususi za mkutano wa 2024, na kuanza michakato yote muhimu ya maandalizi.

## VI. KUHUSU KAMATI NDOGO JUU YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: KUHUSU KUMALIZIKA KWA SERA YA UBIA NA MFUMO WA KIMKAKATI WA AU (AUPPSF) – Doc. EX.CL/1523(XLV)B

**70.** **LINATAMBUA** ukosefu wa makubaliano juu ya masuala ya ugawaji, ushiriki na utoaji majina yanayohusiana na AUPPSF;

**71.** **LINAMUOMBA** Mwenyekiti wa Baraza Kuu na Mwenyekiti wa Kamisheni kufanya mashauriano kwa haraka kuhusu masuala yanayohusiana na Sera ya Ubia na Mfumo wa Kimkakati wa AU na kuwasilisha matokeo ya mashauriano hayo kwa Nchi Wanachama kwa wakati unaofaa.

## UAMUZI KUHUSU

## RIPOTI YA MAENDELEO KUHUSU UTEKELEZAJI WA UAMUZI EX.CL/DEC.1242(XLIV) JUU YA HALI KATIKA BUNGE LA AFRIKA – Doc. EX.CL/1526(XLV)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti ya Kamisheni kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Uamuzi EX.CL/Dec.1242 (XLIV) unaohusu hali ilivyo katika Bunge la Afrika (PAP);

2. **LINAREJEA** maamuzi yake - EX.CL/Dec.1128(XXXIX) wa Oktoba 2021, EX.CL/Dec.1148(XL) wa Februari 2022, EX.CL/Dec.1174(XLI) wa Julai 2022, na EX.CL/Dec.1242 (XLIV) wa Februari 2024 – kuhusu matukio ndani ya PAP;

3. **LINATAMBUA** kwamba masuala yanayojirudia ya kiutawala na kiuendeshaji ambayo yanazuia ufanisi wa Chombo hicho yanapaswa kushughulikiwa ndani ya muktadha mpana wa mchakato wa Mageuzi ya Kitaasisi. **LINATAMBUA ZAIDI** umuhimu wa kuendesha Itifaki ya 2014 ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika (Itifaki ya Malabo) ili kushughulikia changamoto za kiuendeshaji za Chombo hicho;

4. **LINAHIMIZA** Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo kufikiria kusaini, kuridhia, na/au kujiunga na masharti ya Itifaki ya Malabo;

5. **LINAIAGIZA** Kamisherni kutekeleza masuala yaliyosalia ya uamuzi EX.CL/Dec.1242(XLIV) na kutoa ripoti wakati wa Mkutano wa Kawaida ujao wa Baraza Kuu mnamo Februari 2025; na

6. LINAAMUA kuendelea kujadili suala hili.

## UAMUZI KUHUSU ANDIKO DHANA LA KAULIMBIU YA MWAKA 2025, "HAKI KWA WAAFRIKA NA WATU WA ASILI YA KIAFRIKA KUPITIA FIDIA" – Doc. EX.CL/1528(XLV

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.884(XXXVII) wa Februari 2024 ambao ulichagua Kaulimbiu ya Mwaka kwa mwaka 2025 kuwa *"Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Kiafrika Kupitia Fidia"*;

2. **LINAKARIBISHA** Andiko Dhana na Mwongozo kwa ajili ya Kaulimbiu ya Mwaka 2025 vilivyowasilishwa na Kamisheni; **LINAPITISHA** Kaulimbiu ya Mwaka kwa Mwaka 2025 kama *"Haki kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Kiafrika Kupitia Fidia"* na linasisitiza kuwa utekelezaji wa Uamuzi Assembly/AU/Dec.884(XXXVII) ni hatua muhimu katika kupata haki na uponyaji kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Kiafrika, pamoja na kutoa wito wa uwajibikaji kwa makosa ya jinai ya kihistoria na mauaji ya halaiki yaliyofanywa dhidi ya Waafrika na Diaspora ya Afrika duniani; na **LINATOA WITO** wa kupatikana fedha zinazohitajika kwa ajili ya Kaulimbiu ya Mwaka 2025;

3. **LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuzindua Kaulimbiu ya Mwaka 2025 katika nchi zao husika; na **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kutoa rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kaulimbiu ya mwaka katika ngazi ya taifa;

4. **LINAIAGIZA** Kamisheni kuingiza haki ya fidia na uponyaji wa rangi katika utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025;

5. **ZAIDI LINAAGIZA** Vyombo na taasisi husika za AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs), Uwakilishi wa Kudumu wa Nchi Wanachama, na Ofisi Maalum za Kiufundi kuingiza haki ya fidia na uponyaji wa rangi katika programu zao na kusaidia utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025.

6. **LINAIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana kwa karibu na Vyombo na taasisi husika za AU, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025, na kuwasilisha ripoti ya maendeleo kwenye Mkutano wa Uratibu wa Saba (7) wa Nusu Mwaka na Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali mnamo Februari 2026.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA KAMATI MAALUM ZA KIUFUNDI (STCs)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti za Kamati Maalumu za Kiufundi (STCs);

2. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1032(XXXIV) kuhusu kusitishwa kwa uundwaji wa mashirika na ofisimpya;

3. **LINASISITIZA** kuwa uamuzi uliopo haupaswi kuwa na athari zozote za kifedha, kisheria na kimuundo kwa AU na **LINATOA WITO ZAIDI** kwa STCs na mabaraza yote ya mawaziri na vikao vyote vya ufundi kuacha kupitisha miundo au bajeti ambayo haikuzingatiwa na vyombo vya sera kupitia mchakato unaostahili;

4. **LINAOMBA KWAMBA** STC zote zipitishe ripoti zao mwishoni mwa mkutano

### I. KUHUSU KIKAO MAALUM CHA NNE (4) CHA KAMATI MAALUM YA KIUFUNDI KUHUSU VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (STC-YCS-4) TAREHE 9 MACHI 2024, ACCRA, GHANA – Doc. EX.CL/1531(XLV)

**Baraza Kuu,**

5. **LINAZINGATIA RIPOTI** ya Kikao cha Maalumu cha Nne cha Kamati Maalumu ya Kiufundi kuhusu Vijana, Utamaduni na Michezo (STC-YCS4) uliofanyika Accra, Ghana tarehe 09 Machi 2024;

6. **LINAIDHINISHA** ombi la Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kuandaa Michuano ya 14 ya Michezo ya Afrika mwaka2027 kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika (AUSC);

7. **LINAZIOMBA** AUC na STC-YCS kuchukua hatua zinazohitajika endapo hazitatii sheria na masharti kama ilivyoainishwa katika Makubaliano ya Nchi kati ya Umoja wa Afrika na nchi mwenyeji wa Michezo ya Afrika.

8. **AIDHA LINALIOMBA** Baraza la Michezo la AU kufanya kazi kwa karibu na Shirikisho la Vyama vya Michezo Afrika (AASC) na mashirika mengine yote yenye nia sawa na Shirikisho la Michezo Afrika ili kuhakikisha maandalizi ya mapema ya kiufundi na maandalizi ya Michezo ya Afrika kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Michezo la Umojawa Afrika Kifungu cha 18.

9. **LINALISISHI** Baraza la Michezo la AU kupata wakala wa muda mrefu wa masoko na mtangazaji wa Michezo ya Afrika ili kuinua hadhi ya Michezo hiyo na kuleta faida kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (j) cha Kanuni za Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika.

10. **LINAIPONGEZA** Jamhuri ya Ghana kwa kujitolea kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika kuandaa kwa mafanikio Michuano ya 13 ya Michezo ya Afrika mjini Accra, Ghana kuanzia tarehe 08 hadi 23 Machi 2024.

11. **LINAUTANGAZA** mji wa Accra kama mji wa Michezo wa Afrika wa mwaka 2024 hadi Michuano ijayo ya Michezo Afrika.

12. **LINAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutoa umuhimu kwa mchango wa michezo katika kufikia mafanikio ya Ajenda ya AU 2063, Afrika Tunayoitaka na kutenga rasilimali zaidi kwa programu na shughuli za michezo.

## II. KUHUSU KIKAO CHA 4 CHA KAWAIDA CHA KAMATI MAALUM YA UFUNDI YA VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO – Doc. EX.CL/1439(XLIII)

## I. MAAMUZI KUHUSU VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

KUHUSU MAENDELEO YA VIJANA

### i. Wasilisho kuhusu Mjumbe wa Vijana

13. **LINAZINGATIA ZAIDI** mapendekezo ya Mjumbe wa Vijana wa AUC kupitia upya Mkataba wa Vijana, kulingana na Kifungu cha 31 cha Mkataba huo ili kuakisi matarajio yanayobadilika ya Vijana wa Afrika.

14. **LINAIOMBA** Kamisheni kutoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kushughulikia hali halisi inayojitokeza na ya sasa ya Vijana wa Afrika kupitia Mkataba wa Vijana wa Afrika.

15. **LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni ya AU kufanya utafiti na kuchapisha ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa Mkataba wa Vijana wa Afrika tangu kupitishwa.

16. **LINAAMUA** kuanzisha Ofisi ya Mjumbe wa Vijana wa Mwenyekiti wa AUC kwa ajili ya kuhakikisha mwendelezo wa uwakilishi wa sauti za vijana katika uongozi wa Kamisheni ya AU.

17. **LINAZIOMBA** Idara zinazohusika za Kamisheni ya AU kushirikiana na Mjumbe wa Vijana kutathmini athari za kifedha, kisheria na kimuundo za uanzishwaji wa taasisi na kuwasilisha kwa Vyombo vya Sera vinavyohusika ili kujadiliwa.

**ii. Ripoti kuhusu programu ya kuunganisha vijana Afrika, *YouthConnekt Africa***

**18. LINAIOMBA** Kamisheni kuendeleza usaidizi wake kwa Afrika kama jukwaa la shughuli bunifu za maendeleo ya vijana katika Nchi Wanachama kulingana na Mkataba wa Vijana Afrika, Ngazi Inayofuata ya Milioni 1 na Mwongozo wa Mgawanyiko wa Idadi ya Watu kupitia maendeleo ya mifumo husika ya ushirikiano.

**19. LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni ya AU kwa ushirikiano na YouthConnekt Africa kutoa ripoti kuhusu utekelezaji wa uamuzi huu katika kikao kijacho cha STC.

**iii. Kukuza Kujitolea kwa Vijana na Programu za Kitaalamu za Vijana barani Afrika**

**20. LINATHIBITISHA** Sera ya Kitaifa ya Kujitolea ya AU, na Mfumo wa Kujitolea wa AU kama mwongozo wa marejeleo kwa Nchi Wanachama zinazoanzisha au kusasisha sera ya kitaifa ya kujitolea, mkakati au mpango ili kupata msukumo kutokana na kuoanisha juhudi za kitaifa kwenye mifumo ya bara.

**21. LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuwasilisha kwa Kamisheni ya AU ripoti zao za kitaifa kuhusu kujitolea kwa Vijana kwa ajili ya kuendeleza ripoti ya AU ya Hali ya Vijana ya Kujitolea.

**22. LINAPENDEKEZA** kwamba Nchi Wanachama kufadhili raia wao kuhudumu katika mpango wa AU Youth Volunteer Corps kupitia utaratibu uliowekwa wa kuajiri na kupeleka ili kuimarisha ushiriki wa raia wao katika Kikosi cha Vijana cha Kujitolea cha AU.

**23. LINAIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana na na Ofisi ya STC, kuandaa na kuwasilisha mkakati wa kuanzishwa kwa Programu za Kitaalamu za Vijana za AU ili kuzingatiwa na Mkutano Mkuu wa AU na kutoa ripoti mara kwa mara juu ya utekelezaji wa uamuzi huu.

**iv. Mpango wa Ushirikishwaji wa Kifedha na Kiuchumi wa Wanawake na Vijana (WYFEI) wa Mwaka 2030**

**24. LINAZIOMBA** Nchi Wanachama kuunga mkono Mpango wa WYFEI 2030 kwa kuoanisha mikakati ya kitaifa ya uwezeshaji wanawake na vijana, programu, na uwekezaji kwenye Mpango wa WYFEI 2030 na kutumia mbinu hiyo kwa kubadilishana maarifa, mbinu bora, uzoefu, na rasilimali kuelekea kufikia matokeo na kiwango bora.

**v. Uwakilishi Sawa wa Wanawake na Wanaume na Mpango wa idadi ya kikomo ya Vijana**

25. **LINAIOMBA** AUC kushiriki katika juhudi za kuongeza uelewa ili kutangaza Mpango wa AUC wa Uwakilishi Sawa wa Nafasi ya Wanawake na Vijana na kufanya kazi na Nchi Wanachama ili kusaidia utekelezaji wa mipango hiyo kwa kutoa Msaada wa Kiufundi wa Nchi na kujenga uwezo.

III. **KUHUSU KIKAO MAALUM CHA PILI (2) CHA STC KUHUSU MAWASILIANO NATEHAMA – Doc. EX.CL/1532(XLV)**

**Baraza Kuu:**

26. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kikao Maalum cha Pili cha Kamati Maalumu ya Kiufundi ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari na Mawasiliano **(E-STC-CICT)** kilichofanyika kuanzia tarehe 11 hadi 13 Juni 2024 na Tamko la STC-CICT la mwaka 2024;

27. **LINAWAPONGEZA** Mawaziri wenye dhamana ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kufanikisha Kikao cha Kawaida cha Pili cha Kamati yao Maalumu ya Kiufundi (STC) na kupata matokeo muhimu ya maendeleo ya sekta za Mawasiliano, Habari na Mawasiliano Barani Afrika.

28. **LINAPITISHA:**

(a) Mkataba wa Kidijitali wa Kiafrika; na
(b) Mkakati wa Bara wa Akili Bandia (AI).

29. **LINAZIOMBA NCHI WANACHAMA:**

(a) Kusaidia utekelezaji wa Mkataba wa Kidijitali wa Afrika na Mkakati wa Akili Bandia;
(b) Kuwaomba wanadiplomasia wao katika Umoja wa Mataifa kutetea mapendekezo na hatua muhimu katika Mkataba wa Kidijitali wa Kiafrika wakati wa mazungumzo ya Mkataba wa Kidijitali wa Kimataifa na mashauriano katika Mkutano ujao;
(c) Kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika mijadala na mazungumzo ya kimataifa kuhusu usimamizi wa AI na kukuza Mkakati wa Bara la Afrika
(d) Hakikisha upatikanaji wa nishati ili kuwezesha mageuzi ya kidijitali jumuishi.

30. **LINAIOMBA KAMISHENI YA AU**:

(a) Kuandaa Kongamano la Kiafrika kuhusu AI mwaka 2025;
(b) Kujenga juu ya Mkakati wa AI wa Bara ili kukuza Mikakati ya AI katika sekta muhimu.(Elimu, Kilimo, Afya, Viwanda, Amani na Usalama n.k)

(c) Kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mkataba wa Kidijitali wa Kiafrika na Mkakati wa AI wa Bara uliopitishwa.

31. **LINATOA WITO KWA:** Taasisi za fedha za kimataifa, washirika wa maendeleo, na sekta kibinafsi ikiwa ni pamoja na AfDB, Benki ya Dunia na Benki ya Afrexim **Kukusanya** rasilimali ili kutekeleza Mkataba wa Kidijitali wa Afrika na Mkakati wa AI wa Bara.

## IV. KUHUSU KIKAO CHA KAWAIDA CHA SITA (6) CHA STC KUHUSU FEDHA, MAMBO YA FEDHA, MIPANGO YA UCHUMI NA UTANGAMANO (2023) – DOC.EX.CL/1534(XLV)

**Baraza Kuu,**

32. **LINAZINGATIA** na **KUPITISHA** Ripoti na Tamko la Kikao cha 6 cha Kawaida cha Kamati Maalumu ya Kitaalam (STC) kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Uchumi na Utangamano, na mapendekezo yaliyomo;

33. **LINAELEZA** wasiwasi kuhusu kusuasua kutiwa saini na kuidhinishwa kwa hati ya kisheria inayoanzisha Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika (AUFI's);

34. **LINATHIBITISHA TENA** kwamba kufikia Dira na Matarajio adhimu ya Ajenda 2063, kutahitaji mtazamo wenye malengo sawa, wa kina, wa kiujumla na wenye kuleta mageuzi kwa kuzingatia taratibu za ufadhili endelevu zinazosimamiwa na taasisi madhubuti, zinazoweza kuwajibika na shirikishi, sera nzuri na utawala bora katika ngazi zote;

35. **LINATHIBITISHA ZAIDI** azimio lake la kuhakikisha kwamba mabadiliko ya Afrika, ukuaji wa viwanda na mseto wa kiuchumi unafadhiliwa kwa njia inayotabirika, endelevu, yenye usawa na uwajibikaji na umiliki kamili wa Nchi Wanachama wake;

36. **LINAAMUA** yafuatayo:

a) **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama wote kufanya kazi kwa ari mpya katika kutia saini na kuridhia vyombo vya kisheria vya Mfuko wa Fedha wa Afrika na Benki ya Uwekezaji ya Afrika pamoja na kufikia muafaka wa viwango vya mtaji wao wa awali ili Kikao Maalum cha Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika waliojitolea kipekee kwa uanzishwaji wa Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika kuitishwa kabla ya mwisho wa mwaka 2024;

b) **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuharakisha kukamilisha utafiti wa kitaalam kuhusu Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika katika muktadha wa sasa wa kiuchumi na kifedha wa Nchi Wanachama ili kushughulikia masuala yote ya kitaalam yanayohusu uanzishwaji wa AUFIs;

c) **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kufanya kazi kwa karibu na Muungano wa Benki Kuu za Afrika na Nchi Wanachama ili kuhakikisha kwamba michakato yote ya kitaasisi na kiufundi inayosubiri kuanzishwa kwa Taasisi ya Fedha ya Afrika inatekelezwa kabla ya mwisho wa mwaka 2024 na matokeo ya ushirikishaji huo uwe sehemu ya Ripoti ya Mwamasishaji kwenye Mkutano Mkuu mwaka 2025;

d) **LINAIOMBA ZAIDI** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Kubadilishana Dhamana Afrika (ASEA) kwa uhamasishaji wa kimkakati wa rasilimali kwa nia ya kuimarisha na kuongeza Mradi wa Uhusiano wa Masoko ya Afrika (AELP) kuelekea mageuzi yake kama Soko la Hisa la Afrika (PASE) na **LINAAMUA** kuwa matokeo ya ushirikiano huo yawe sehemu ya Ripoti ya Mhamasishaji kwenye Mkutano Mkuu mwaka 2025;

e) **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Benki ya *African Export Import Bank*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Taasisi nyingine za Kimataifa za Kifedha za Afrika na Tume ya Kiuchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika kutoa msaada ufaao wa kiufundi na kifedha kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa ajili ya uendeshaji wa haraka wa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika; na

f) **PIA LINATOA WITO KWA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Chama cha Benki Kuu za Afrika na Mfumo wa Mapitio ya Utawala Bora Afrika kuanza zoezi la Mapitio ya Utawala Bora kwa Nchi Wanachama kwa nia ya kuhimiza utekelezaji wa vigezo vya umoja wa uchumi jumla ili kuruhusu ufuatiliaji wa njia yetu kuelekea kwenye sarafu moja Afrika na **LINAZITAKA** Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kuzitumia kwa uangalifu;

**Utekelezaji wa Hatua Muhimu za Kusaidia kuharakisha mageuzi ya Afrika kuelekea Uanzishwaji wa Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika**

**A. Kuhusu ukusanyaji wa rasilimali za ndani na nje:**

**37.** **LINAPONGEZA** Kundi la Afrika, Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama wa AU kwa juhudi zao za kupiga kura ya kihistoria juu ya Azimio lililoungwa mkono na Nigeria kwa niaba ya Kundi la Afrika wakati wa mijadala ya Kamati ya Pili mnamo Novemba 22, 2023 ili kufanikisha mageuzi ya kina ya mfumo wa kimataifa wa kodi chini ya Umoja wa Mataifa ambayo yangehakikisha muundo wa kodi ambao ni jumuishi, wa wazi na unaofaa kwa ajili ya madhumuni ya maendeleo ambao unalinda haki za kodi za nchi zote;

**38.** **LINAITAKA** Kamisheni kuongeza uungaji mkono wake wa kiufundi kwa Kikosi Kazi za Afrika na kuhamasisha uzito wa kisiasa na uongozi ili kupata kasi ya sasa kuelekea muundo wa kodi wa kimataifa jumuishi na wa wazi zaidi;

39. **LINATOA SHUKRANI ZA DHATI** kwa nchi zote ambazo tayari zimeonesha kuunga mkono Marekebisho ya Muundo wa Kodi wa Kimataifa katika Umoja wa Mataifa;

40. **LINATOA WITO** kwa nchi ambazo zimepiga kura kupinga rasimu ya azimio kuunga mkono mchakato wa sasa kwa moyo wa kibinadamu kwa ustawi na maendeleo ya pamoja.

41. **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Jukwaa la Udhibiti wa Kodi Afrika, Mtandao wa Usawa wa Kodi, na Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika kwa msaada wa washirika kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama kwa nijia ya kujenga uwezo na usaidizi wa kiufundi ili kuimarisha uhamasishaji wa rasilimali za ndani na kuzuia mtiririko wa fedha haramu kwa lengo la kusaidia utekelezaji wa miradi na programu za Agenda 2063.

**B. Utafiti kuhusu Hatua Muhimu za Kufikia Ukuaji Shirikishi na Maendeleo Endelevu Barani Afrika**

42. **LINAZINGATIA** ripoti ya matokeo muhimu ya Utafiti na **KUPONGEZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) kwa kukamilisha Utafiti juu ya Ukuaji Jumuishi na Endelevu; na **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama kuidhinisha na kutekeleza hatua na sera muhimu zilizopendekezwa kwa nia ya kufikia viwango endelevu vya ukuaji wa uchumi wa kila mwaka wa asilimia 7-10 katika miongo ijayo ili kuhakikisha kufanikiwa kwa Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika 2063.

43. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Taasisi za Afrika nzima na washirika kuunga mkono utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo ndani ya ripoti.

44. **LINAISIHI** Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD) kubuni na kutekeleza mchakato wa ufuatiliaji na tathmini wa ufanisi na ufanisi ili kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa hatua muhimu zilizopendekezwa kwenye Utafiti huo.

45. **LINAIOMBA** Kamisheni kuwasilisha ripoti ijayo kuhusu hali ilivyo kwa Baraza Kuu mwaka 2025.

**C. Kikundi Kazi cha Ngazi ya Juu kuhusu Mustakabali wa Muundo wa Fedha Duniani**

46. **LINAZINGATIA** shughuli zinazoendelea za Kikundi Kazi cha Ngazi ya Juu kuhusu Mustakabali wa Usanifu wa Kifedha Duniani;

47. **LINATOA WITO** kwa Kamisheni ya AU kuingiza kazi ya Kikundi Kazi cha Ngazi ya Juu katika vyombo vya sera vya AU kupitia Kamati Maalumu ya Kiufundi ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano;

**48. LINAISIHI** Kamisheni ya AU na Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika kufanya kazi kwa pamoja ili kuunganisha na kutetea Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Marekebisho ya Usanifu wa Kifedha Duniani wenye hoja za kimkakati na mazungumzo yaliyo wazi;

**49. LINAKISIHI ZAIDI** Kikundi Kazi cha Ngazi ya Juu kujumuisha mageuzi ya usanifu wa kimataifa wa kodi katika kazi zake; na

**50. LINAKIOMBA** Kikundi Kazi kuendelea kuwasilisha ripoti yao ya maendeleo ya kila mwaka kwa Kamati Maalumu ya Kitaalam ya Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano, ambayo itakuwa sehemu ya ripoti ya mwaka ya Mwamasishaji kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU mwaka 2025.

**D. Maendeleo Yanayoibuka: Kiti cha Kudumu cha Umoja wa Afrika katika Kundi la 20 (G20)**

**51. LINAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.845(XXXVI) wa Kikao cha Kawaida 36 cha Mkutano Mkuu kilichofanyika kuanzia tarehe 18-19 Februari 2023, Addis Ababa, Ethiopia; na **LINAKARIBISHA** uamuzi wa Viongozi wa mkutano wa G20 mjini New Delhi uliofanyika kuanzia tarehe 9 hadi 10 Septemba 2023 chini ya kaulimbiu 'Dunia Moja, Familia Moja, Mustakabali MMoja' kutoa uanachama wa kudumu kwa Umoja wa Afrika katika G20.

**52. LINAHIMIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kubuni mbinu zilizo wazi na kufafanua majukumu mahususi na mgawanyo wazi wa kazi kwa Kamisheni, Mawaziri wa Fedha, Magavana wa Benki Kuu, Mashirika Maalumu ya AU, na wadau wengine.

**53. PIA INAHIMIZA** Kamisheni kufafanua kwa uwazi matarajio ya kimkakati kwa bara kutumia uwezo wa G20.

**E. Kushughulikia Mashirika ya Kimataifa ya Kifedha ya Afrika (AMFIs) katika Utatuzi wa Deni la Afrika**

**54. LINAZISIHI** Nchi Wanachama kuthibitisha jukumu kuu la AMFIs kama taasisi za kimataifa zinazomilikiwa na Afrika ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya bara;

**55. LINAZISIHI ZAIDI** Nchi Wanachama kuheshimu wajibu wa Mkataba kwa Taasisi za Fedha za Kimataifa za Afrika katika mazungumzo ya madeni na Benki za Maendeleo za Kimataifa (MDBs) na taasisi zingine;

**56. LINAMUOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kutoa barua kwa Benki za Maendeleo ya Kimataifa (MDBs) na taasisi nyingine, kwa kushauriana na Ofisi ya Washauri wa Kisheria kuangazia wasiwasi wa Nchi Wanachama juu ya suala hili na kuzitaka kuainisha na kuzichukulia AMFIs kama wakopeshaji wa

pande nyingi wakati wa mazungumzo yao kuhusu madeni na watawala wa Kiafrika, kulingana na majukumu yao ya Kimkataba;

57. **LINAAMUA** kuunda Klabu ya Afrika, kundi lisilo rasmi linaloundwa na Taasisi za Kifedha za Kimataifa za Afrika (AMFIs) kama jukwaa lililojitolea la bara la wadai rasmi wa Kiafrika ili kupata suluhu zilizoratibiwa na endelevu kwa matatizo ya ulipaji wa madeni yanayozikabili Nchi Wanachama; na

58. **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa msaada wa AMFIs kuandaa mkutano wa bara juu ya utatuzi wa madeni Afrika mwaka 2024 na kutoa ripoti kwa Tasisi za Sera za Umoja wa Afrka.

**F. Taarifa kuhusu Kuanzishwa kwa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo Afrika**

59. **LINAZINGATIA** kuidhinishwa kwa Kamati Maalumu ya 6 ya Kitaalamu Fedha, Masuala ya Kifedha, Mipango ya Kiuchumi, na Kujumuishwa kwa pendekezo lililotolewa na APRM la kuanzishwa kwa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo wa Kiafrika unaoendeshwa na sekta binafsi kwa msingi wa kujifadhili na kujiendeleza;

60. **LINAIOMBA** AUC-PRM kwa kushirikiana na AfreximBank na Mashirika mengine ya Kifedha ya Mshikamano wa Afrika kuharakisha utendaji wa Wakala wa Ukadiriaji wa Mikopo wa Afrika unaoendeshwa na sekta binafsi kwa kuzingatia ufadhili binafsi; na

61. **LINAOMBA ZAIDI** APRM, UNECA na AUC kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya ukadiriaji wa mikopo na taasisi za kiufundi kuhusu usambazaji wa data na viwango vya uwazi katika kuimarisha ukadiriaji wa mikopo barani Afrika.

## V. KUHUSU KIKAO CHA 4 CHA KAWAIDA CHA KAMATI MAALUM YA UFUNDI YA BIASHARA, UTALII, VIWANDA NA MADINI – Doc. EX.CL/1535(XLV)

**Baraza Kuu,**

62. **LINAKARIBISHA** kuitishwa kwa Mkutano wa 4 wa Kamati Maalumu ya Kiufundi ya Biashara, Utalii, Viwanda na Madini uliofanyika Malabo, Jamhuri ya Guinea ya Ikweta kuanzia tarehe 16 hadi 17 Mei 2024 chini ya kaulimbiu *“Kuimarisha Ushindani wa Biashara wa Afrika Kupitia Utalii, Maendeleo ya Rasilimali za Viwanda na Madini.”*

63. **LINAZINGATIA** Ripoti na Tamko la Mkutano wa 4 wa Kamati Maalum ya Kiufundi ya Biashara, Utalii, Viwanda na Madini na matokeo yaliyomo, kama yalivyoambatanishwa.

64. **LINAZINGATIA** Kanuni zilizoboreshwa za Uendeshaji wa Kamati Maalumu ya Kiufundi ya Biashara, Utalii, Viwanda na Madini na **KUIAGIZA** Kamati

Maalumu ya Kiufundi ya Haki na Masuala ya Sheria kukamilisha hilo kwa kufutwa kisheria na kuwasilisha hivyo kwenye Mkutano wetu ujao. Februari 2025 kwa uidhinishaji.

**65.** **LINAKARIBISHA** kuundwa kwa Kamati Ndogo Nne (4) za STC - TTIM zitakazoundwa na wawakilishi wa Nchi Wanachama kutoka miji mikuu inayozingatia kila eneo, yaaniBiashara, Utalii, Viwanda na Madini.

**66.** **LINAKARIBISHA** uundwaji wa Mkakati wa Madini ya Kijani Afrika na **KUIOMBA** STC-TTIM kukamilisha kuzingatia na kupitishwa kwa Mkakati huo na kuuwasilisha kwenye mkutano wetu ujao mwezi Februari 2025 kwa ajili ya kuidhinishwa.

**67.** **LINAIDHINISHA** Mikakati na Mifumo ifuatayo inayolenga kuimarisha ushindani wa kibiashara barani Afrika kupitia Utalii, Maendeleo ya Viwanda na Rasilimali Madini:

(i) Mkakati wa Biashara ya Mtandao wa Umoja wa Afrika
(ii) Mfumo wa Sera ya Kuanzisha Umoja wa Afrika.
(iii) Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau wa Umoja wa Afrika kama mwongozo wa uundaji waSera za Biashara barani Afrika.
(iv) Mwongozo wa Udhibiti wa Kiufundi wa Bara la Afrika (ACTReF);
(v) Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Mitindo na Mfumo wa Udhibiti wa Mpango wa Mitindo wa Pan African
(vi) Fasili ya Umoja wa Afrika ya Biashara Ndogo zaidi, Ndogo na za Kati.

**68.** **LINAIDHINISHA** Uamuzi kuhusu Utaratibu wa Kurekebisha Mipaka ya Kaboni (CBAM) na **LINAIOMBA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika na washirika wake kufanya utafiti wa kina juu ya athari za ushuru wa kaboni kwenye ushindani wa bidhaa nahuduma za Kiafrika.

**69.** **LINAKARIBISHA** kuanzishwa kwa mpango wa Madaraja ya Biashara kati ya Nchi za Kiarabu na Afrika kama jukwaa la ushirikiano kwa ajili ya upanuzi na maendeleo ya biashara na uwekezaji baina ya pande hizo kwa ajili ya kukuza maendeleo ya biashara, uwekezaji, Bima, na Miundombinu kati ya nchi za Kiarabuna Kiafrika.

**70.** **LINAIAGIZA** Kamisheni kwa kushirikiana na washirika na wadau husika kuunga mkonoutekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti na Tamko.

**71.** **LINAISHUKURU** Serikali na Watu wa Jamhuri ya Equatorial Guinea kwa kuandaa Mkutano wa 4 wa STC-TTIM.

## VI. KUHUSU RIPOTI YA MKUTANO WA KAWAIDA WA 16 WA KAMATI MAALUM YA KIUFUNDI KUHUSU ULINZI NA USALAMA- Doc. EX.CL/1533(XLV)

**Baraza Kuu,**

**72.** **LINAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa Kawaida wa 16 wa Kamati Maalum ya Kiufundi kuhusu Ulinzi na Usalama (STCDSS) uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 3 hadi 5 Juni 2024; na **LINAIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani ya ripoti;

**73.** **LINAIDHINISHA** Dhana ya Kimkakati ya Umoja wa Afrika *African Union Strategic Lift Concept*, iliyopitishwa na Mkutano wa Kawada wa STCDSS, na **LINAZISIHI** Nchi Wanachama kudhamiria kutoa nafasi ya kimkakati, ardhi na vikosi saidizi vya baharini kama sehemu ya uendeshaji wa ASF pamoja na ujumbe wa kiutu na misaada wakati wa matukio ya majanga ya asili, kwa kuzingatia kazi ongozi ya vyombo vya RECS/RMs katika aina fulani ya harakati;

**74.** **LINAIDHINISHA** Mwongozo wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya Usimamizi wa Opresheni za Kusaidia amani, ambao ulipitishwa na Mkutano wa Kawaida wa STCDSS, na **LINAZINGATIA** umuhimu wa kufafanua ulinzi wa wafanyakazi wa PSO dhidi ya madai hayo kwa kufanya utafiti wa kina na kuangazia kutokana na madai, na kudai pia udanganyifu katika utafiti na kuangazia tuhuma za usiri hadi uchunguzi utakapokamilika;

**75.** **LINAPITISHA** Sera ya Mafunzo ya Umoja wa Afrika kwa ajili ya Operesheni za Kusaidia Amani, iliyopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 16 wa STCDSS, na **KUIOMBA** Kamisheni kuanzisha ubia na Nchi Wanachama wa AU ili kuoanisha mafunzo na kuandaa kanzidata ya mafunzo ya PSOs yanayoptaikana barani;

**76.** **LINAIOMBA** Kamisheni kutengeneza ramani ya njia ya kina na jumuishi kwa ajili ya mapitio mapana ya Kikosi cha Utayari cha Afrika (ASF) na kuwasilisha matokeo na mapendekezo ya mapitio kwenye Mkutano wa Kawaida wa 17 wa STCDSS.

**77.** **LINAIOMBA** Kamisheni ya AU, kwa uratibu na Baraza la Amani na Usalama, Wajumbe wa Afrija kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na wadau wengine wanaohusika, kuchambua Azimio Na. 2718 (2023) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwezesha utekelezaji wake na kuanzisha mara moja chombo cha kimkakati kukusanya asilimia 25 iliyobakia kwa ajili ya kugharamia operesheni ya kusaidia Amani katika muktadha wa utekelezaji wa Azimio hilo.

**UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA TIMU HURU YA UFUNDI YA AU JUU YA KUWA MWENYEJI WA SHIRIKA LA KIBINADANAMU WA AFRIKA (AfHA) – Doc. EX.CL/1538(XLV)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.856(XXXVI) uliopitisha Sheria ya Wakala wa Kiutu Afrika (AfHA), pamoja na Kifungu cha 8 cha Sheria hiyo kinachosema kwamba Kiti cha AfHA kitaamuliwa na Mkutano Mkuu baada ya wito wa maombi ya kugombea;

2. **LINAZINGATIA** ripoti ya tathmini ya kiufundi ya Kamisheni juu ya kuwa mwenyeji wa AfHA na **LINAPONGEZA** kazi kubwa na ya kitaalamu inayofanywa na Timu ya Tathmini ya Kiufundi;

3. **AIDHA LINAZIPONGEZA** Nchi nne (4) Wanachama zilizojitolea kuhodhi AfHA kwa kujitolea kwao na kiwango cha kujitolea kinachoonyeshwa katika mchakato mzima wa tathmini;

4. **LINAPENDEKEZA** kwa Mkutano Mkuu kuteua Jamhuri ya Uganda kama Nchi mwenyeji wa AfHA;

5. **LINAIOMBA** Kamisheni kuendelea kusaidia utekelezaji kamilifu wa AfHA mapema iwezekanavyo;

6. **LINATOA WITO** kwa Nchi Wanachama, wabia wa Maendeleo, na wadau wa sekta binafsi barani Afrika kuunga mkono uharakishaji wa utekelezaji wa AfHA, ikiwa ni pamoja na kutimiza ahadi zilizotolewa wakati wa Mkutano Maalum wa 15 wa Kibinadamu na Mkutano wa Ahadi, uliofanyika tarehe 27 Mei 2022, Malabo, Equatorial Guinea.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MWENYEKITI WA KAMISHENI JUU YA UENDESHAJI WA MFUKO WA AMANI WA UMOJA WA AFRIKA.

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** ripoti na **KUIPONGEZA** Kamisheni ya AU kwa hatua iliyofikiwa katika uendeshaji wa Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika, kwa maana ya, kuweka muundo wa utawala na utoaji wa rasilimali za fedha kupitia Mfuko wa Akiba wa Migogoro (CRF) na miradi ya majaribio ya kushughulikia changamoto za usalama barani Afrika.

2. **LINAREJEA** uamuzi EX.CL/ Dec.1223(XLIII) aya ya 31, uliochukuliwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Baraza Kuu mnamo Julai 2023 uliofanyika mjini Nairobi, ambao uliomba Kamisheni kupitia Sekretarieti ya Mfuko wa Amani kuchunguza mbinu za kupata michango ya hiari kutoka kwa Nchi Wanachama pamoja na michango kutoka kwa sekta binafsi na **LINAHIMIZA** Sekretarieti ya Mfuko wa Amani wa AU, kupeleka juhudi zote katika kukusanya rasilimali za ziada kupitia michango ya hiari ya Nchi Wanachama, kwa kushirikiana na sekta binafsi, watu binafsi wenye utajiri mkubwa na raia wa bara letu.

3. **LINAZINGATIA** hatua iliyofikiwa hadi sasa katika kushirikiana na sekta binafsi ya Afrika, taasisi za fedha za kimataifa, mashirika, mashirika ya serikali, watu binafsi wenye utajiri mkubwa na mabilionea kwa mtazamo wa kukusanya rasilimali kwa ajili ya Mfuko wa Amani na **LINAIHIMIZA** kamisheni kupanua wigo wake kwa upana zaidi kwa nchi wanachama kwa kufuata ipasavyo Sheria za Fedha za AU

4. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama ambazo bado hazijatimiza ahadi zao za fedha kwa Mfuko wa Amani kutimiza ahadi zao.

5. **LINAIOMBA** Kamisheni kukamilisha uendeshaji wa Kikundi Huru cha Tathmini na kufanya mchakato wa uteuzi kupitia Jopo la Waafrika Mashuhuri ili kuhakikisha uwazi.

6. **LINAIAGIZA** Sekretarieti ya Mfuko wa Amani kukamilisha na kuwasilisha Mkakati wa Ukusanyaji wa Rasilimali kupitia utaalamu wa ndani na rasilimali.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KWANZA YA KAMISHENI KUHUSU USHIRIKI WA AU KWENYE G20

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** kazi iliyofanywa na Tume katika kutekeleza Uamuzi wa Mkutano Mkuu Na. Assembly/AU/Dec.873(XXXVII) na Uamuzi wa Baraza Kuu Na. EX.CL/1255(XLIV) uiliopitishwa mwezi February 2024 kuhusu namna ya kushiriki na vipaumbele vya Umoja wa Afrika kwenye G20;

2. **LINAZINGATIA ZAIDI** masuala muhimu kwenye G20, ambayo yana manufaa kwa Umoja wa Afrika, ambayo ni: Kukomesha Njaa na Umaskini; Hatua ya hali ya hewa; Maendeleo ya uchumi-bayolojia; Dijitali na Akili Bandia; Urekebishaji wa Madeni na urekebishaji wa Mfumo wa Pamoja wa G20 juu ya Kushughulikia Madeni; Upya wa SDR na Uhamasishaji wa Ufadhili wa Masharti kwa ajili ya Maendeleo; Marekebisho ya Benki za Maendeleo ya Kimataifa; Marekebisho ya mfumo wa sasa wa utawala wa kimataifa ili kuimarisha ujumuishi na ufanisi wake, Mpito wa Nishati na Ongezeko la Thamani la Madini ya Kijani ya Kiafrika; Ushirikiano wa Kimataifa wa Ushuru; Mshikamano na Afrika; na Afya;

3. **LINAIOMBA** Kamisheni kuwezesha taarifa fupi za robo mwaka kwa Kamati Ndogo ya PRC ya Masuala ya Kiuchumi na Biashara kuhusu ushiriki wa Umoja wa Afrika kwenye G20 ili kuimarisha uratibu wa misimamo na Nchi Wanachama;

4. **LINATHIBITISHA** msimamo kwamba Umoja wa Afrika utajigharamia wenyewe kwa kusaidiana na Taasisi za Kifedha za Umoja wa Afrika katika ushiriki wa G20 kuhakikisha uhuru wake wa pamoja;

5. **LINAAMUA** kufanya Mkutano Maalum kwa njia ya Mtandao wa Baraza Kuu utakachofanyika mwezi Oktoba 2024, ukitanguliwa na mikutano ya Kamati Ndogo ya PRC ya Jumla kuhusu Masuala ya Kiuchumi na Biashara na PRC kujadili rasimu ya misimamo itakayowasilishwa na Mratibu (*Sherpa*) na Mratibu Msaidizi (*Sous-Sherpa*) wa mkutano wa AU wakati wa kujadili Rasimu ya Tamko la Viongozi wa G20 ya mwaka 2024.

6. **LINATOA WITO** kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kabla ya Kikao Maalum cha Baraza Kuu, kuja na nyaraka ya kina kuhusu muundo wa ofisi za Kamati Maalum za Kiufundi;

7. **LINATOA WITO ZAIDI** kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kabla ya Kikao

Maalum cha Baraza Kuu, kuja na dashibodi ya misimamo ya kisera na vipaumbele vya Umoja wa Afrika kwa kuzingatia nyaraka za sera zilizopitishwa;

8. **LINAIOMBA** Kamisheni kusambaza kwa Nchi Wanachama orodha ya Washiriki wa AU kwenye mikutano ya G20 kuanzia tarehe 1 Desemba, 2003 hadi Mei, 2024 pamoja na saraka ya wawakilishi wa AU kwenye mikutano ya G20 pamoja na kalenda ya mikutano ya G20;

9. **LINARUDIA HAJA** ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuja na nyaraka ya sera kama ilivyoamuliwa kupitia Uamuzi wa Baraza Kuu Ex.2/Dec. 1255 (XLIV) wa tarehe 14-15 Februari mara tu Mratibu wa mkutano wa Brazil G20 atakaposambaza rasimu ya awali ya Tamko la Viongozi wa G20 la mwaka 2024; na

10. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama na Kanda ambazo bado hazijafanya hivyo, kuteua wawakilishi wao kwa nafasi ya Wenyeviti wa Kamati Maalumu za Kiufundi za AU na **KUAMUA** kwamba kama hakuna Mwenyekiti aliyechaguliwa wa Kamati ya Kiufundi, mjumbe wa kitengo hicho aombwe na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kushiriki mkutano husika wa Mawaziri wa G20.

# UAMUZI KUHUSU
# RIPOTI YA KIKAO CHA PAMOJA CHA KAMATI YA WAZIRI YA KIPIMO CHA TATHMINI NA MICHANGO NA KAMATI YA MAWAZIRI KUMI NA TANO WA FEDHA (F15)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kikao cha Pamoja kati ya Kamati ya Mawaziri ya Kipimo cha Tathmini na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15) kilichofanyika tarehe 12 Julai 2024.

   a. **Kuhusu Hali ya Michango ya Nchi Wanachama kwenye Bajeti ya Kawaida na Mfuko wa Amani:**

2. **LINAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) wa Februari 2021 mjini Addis Ababa, Ethiopia, ambapo Mkutano huo uliamua kukasimu madaraka yake kwa Baraza Kuu, kutumia Taratibu za Vikwazo vya AU, kwa mujibu wa vipengele vya Ibara ya 23 (1) ya Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika na Kanuni ya 36 ya Sheria za Taratibu za Mkutano Mkuu.

3. **LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia **dola za Marekani 133,101,285.53,** sawa na **asilimia 67** ya dola **za Marekani 200,000,000** ya mchango uliotathminiwa kwa ajili ya Bajeti ya kawaida ya mwaka 2024.

4. **PIA LINAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa kuchangia **dola za Marekani 341,188,642.79** kwa ajili Mfuko wa Amani wa AU tangu mwaka 2017, jambo linaloonesha dhamira ya hali ya juu Umoja huo katika kuendesha Mfuko huo kikamilifu.

5. **LINAZIPONGEZA ZAIDI** Nchi Wanachama ambazo zimetoa michango kikamilifu kulingana na tathmini zao za mwaka 2024 na **KUZIOMBA** Nchi Wanachama kulipa michango yao iliyotathminiwa kwa kuzingatia Kanuni ya 23(1) ya Sheria za Fedha za AU, kwa kuzingatia tofauti za miaka ya fedha ya Nchi Wanachama.

6. **LINAAMUA** kuweka vikwazo kwa Nchi Wanachama zifuatazo ambazo zimerudi nyuma katika kulipa michango yao iliyotathminiwa:

   a. **Vikwazo vya onyo:** Nigeria, Cameroon, Chad, Congo, Madagascar, Benin, Malawi, Eswatini, Lesotho, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Djibouti, Guinea Bissau, Uganda, Niger, Comoro, Gabon, Equatorial Guinea, Burkina Faso, Msumbiji, Senegal, Libya, na Sudan Kusini.

   b. **Vikwazo vya kati:** Mali na Liberia

   c. **Vikwazo vya kina:** Guinea, Sao Tome na Principe

7. **LINAZINGATIA** kwa masikitiko kuwa Nchi Wanachama ishirini na sita (26) wamependekezwa kwa ajili ya vikwazo na, kuhusiana na hili, **LINAMUAGIZA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuwasiliana na kila mojawapo ya Nchi hizi Wanachama kulipa kwa haraka michango yao iliyotathminiwa ili kuruhusu kuondolewa kwa vikwazo vya kifedha.

8. **LINAIELEKEZA** Kamisheni kuandaa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujadiliwa na Kikao cha Pamoja cha Mawaziri kuhusu malipo ya sehemu ya michango ya Nchi Wanachama iliyotathminiwa kwa kutumia sarafu za Kitaifa ili kujadiliwa na Vyombo vya Sera mwezi Februari 2025.

**b. Kuhusu Nchi Wanachama zinazokabiliwa na hali ngumu inayozifanya zishindwe kwa muda kulipa michango yao iliyokadiriwa.**

9. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1071(XXXV) wa Julai 2019 ambao ulizingatia hali ya usalama na kisiasa ya Somalia na Libya na kuzuia vikwazo kwa kutolipa michango yao, na kuiomba Kamisheni kushauriana na nchi hizo mbili ili kukubaliana juu ya utaratibu wa kulipa malimbikizo ya michango yao ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo.

10. **LINAREJEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU/Dec.752(XXXIII) wa mwezi Februari 2020 ambao ulizingatia maombi ya Jamhuri ya Burundi na changamoto ambazo nchi hiyo inakabiliana nazo katika kulipa michango yake ya kila mwaka kwa Umoja huo, na kuiomba Kamisheni kujadiliana na Nchi Wanachama zinazokabiliwa na changamoto katika kulipa michango yao kwa Umoja huo na zile zinazodaiwa kwa muda wa miaka miwili (2) au zaidi ili kukubaliana juu ya utaratibu wa kulipa malimbikizo ya michango yao.

11. **PIA LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1119(XXXVIII) wa Februari 2021 ambao ulizingatia ombi la Jamhuri ya Sudan kuhusu haja ya kupitia mchango wake uliotathminiwa na kuiomba Kamisheni kushauriana na Jamhuri ya Sudan kwa kuzingatia Kipimo cha Tathmini cha sasa ili kukubaliana juu ya Utaratibu wa kulipa malimbikizo yake haraka iwezekanavyo, ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo.

12. **LINAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) wa Februari 2021 ambao uliidhinisha utaratibu wa malipo kwa Jamhuri ya Somalia na Jamhuri ya Burundi kulipa malimbikizo yao.

13. **LINAREJEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU/Dec.838(XXXV) wa Februari 2022 ambapo liliamua kipekee na kwa kuzingatia hali tete ya muda mrefu nchini Libya kwamba baada ya kulipa kikamilifu asilimia 50 ya malimbikizo yake, Kamisheni itafuta asilimia 50 ya michango yake kwa bajeti ya kawaida ya Umoja huo.

14. **LINAREJEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1263(XLIV) wa Februari 2024 ambapo Baraza Kuu, baada ya kuzingatia Taarifa ya Kikao cha Pamoja cha Kamati ya Mawaziri ya Kipimo cha Tathmini na Michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha ( F15) kilichofanyika tarehe 9 Februari 2024, liliipongeza Libya kwa kulipa malimbikizo yake yote na kulipa michango yake iliyotathminiwa kwa mwaka 2023 kwa ukamilifu, ikiwa ni pamoja na michango yote ambayo bado haijalipwa kwa ajili ya Mfuko wa Amani, hali ambayo ilionesha umiliki na dhamira ya kufadhili Umoja wa Afrika kwa njia endelevu.

15. **LINAZINGATIA** kwamba mwaka 2024 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa taratibu za malipo zilizokubaliwa kati ya Kamisheni, Jamhuri ya Somalia na Jamhuri ya Burundi ili kulipa malimbikizo ya madeni kwa umoja wa Afrika, **LINATOA SHUKRANI** kwa juhudi zinazofanywa na Nchi hizo mbili Wanachama kulipa malimbikizo yao kwa Umoja huo na **LINAZIHIMIZA** kuendelea kulipa michango yao kulingana na utaratibu wa malipo uliokubaliwa.

16. **LINAZINGATIA** ombi la Jamhuri ya Somalia la kufanyia marekebisho utaratibu wake wa malipo na **LINAIOMBA** Kamisheni na Jamhuri ya Somalia kukubaliana kuhusu utaratibu wa malipo uliorekebishwa na kutoa ripoti kwa Baraza Kuu mnamo Februari 2025.

17. **LINATHIBITISHA** Uamuzi wake EX.CL/Dec.1119(XXXVIII) wa Februari 2021, na **KWA KUTAMBUA** changamoto kubwa za kisiasa na kiusalama ambazo Sudan inaendelea kukabiliana nazo, **LINAIOMBA** Kamisheni kuwasilisha ripoti kuhusu ya hali ilivyo kwa Baraza Kuu katika kikao chake cha Februari 2025, ikiwa ni pamoja na hatua zilizochukuliwa kukubaliana juu ya utaratibu wa malipo na Sudan, kwa ajili ya kujadiliwa zaidi na kufanya Uamuzi.

# UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MAJAJI WATATU (3) WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA HAKI ZA WATU (AfCHPR) – Doc. EX.CL/1542(XLV)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Majaji Watatu (3) wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu; na

2. **LINAWACHAGUA NA KUWATEUA** wafuatao kama majaji wa AfCHPR kwa kipindi cha miaka **sita** (6):

| NA. | JINA | JINSIA | NCHI | KANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Blaise Tchikaya | Mwanaume | Kongo | Kati |
| 2 | Duncan Gaswaga | Mwanaume | Uganda | Mashariki |
| 3 | Stella Isibhakhomen Anukam | Mwanamke | Nigeria | Magharibi |

# UAMUZI KUHUSU CHAGUZI NA UTEUZI WA RAIS WA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA AFRIKA (PAU) – Doc.EX.CL/1543(XLV)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Rais wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afrika (PAU); na

2. **LINAMCHAGUA TENA NA KUMTEUA** afuataye kuwa Rais wa Baraza la PAU kwa muhula wa miaka mitatu (3), kuanzia Oktoba 2024.

| NA | JINA | JINSIA | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|---|---|
| | Kenneth Kamwi Matengu | Mwanaume | Namibia | Kusini |

**UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA WAJUMBE WAWILI (2) WA BARAZA LA ANGA AFRIKA – Doc. EX.CL/1544(XLV)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Wajumbe Wawili (2) waBaraza la Anga la Afrika;

2. **LINAMCHAGUA NA KUMTEUA** afuataye kama Mjumbe wa Baraza la Anga laAfrika kwa kipindi cha **miaka minne** (4):

| NA. | JINA | JINSIA | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fernand Guy Isseri | Mwanaume | Cameroon | Kati |

3. **LINAAMUA** kuahirisha uchaguzi na uteuzi wa mjumbe mwanamke mmoja (1) wa Baraza la Anga kutoka Ukanda wa Kati mpaka Mkutano wa Kawaida wa arobaini na sita wa Baraza Kuu utakaofanyika mwezi Februari 2025;

4. **LINAZISIHI** Nchi Wanachama wa Ukanda wa Kati kuwasilisha maombi ya wagombea wanawake kwa ajili ya Baraza la Anga; na

5. **LINAIOMBA** Kamisheni kuhalalisha nyaraka za uteuzi za Wajumbe Waliochaguliwa wa Baraza la Anga la Afrika kwa mujibu wa Uamuzi 1256 (XLIV) wa Februari 2024 na kuharakisha masuala ya kiutawala na kifedha kwa kuendana na muundo wa Wakala ili kuufanya ufanye kazi kikamilifu.

# UAMUZI KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MJUMBE MMOJA (1) WA BODI YA USHAURI YA UMOJA WA AFRIKA DHIDI YA RUSHWA (AUABC) – DOC. EX.CL/1545(XLV)

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Mjumbe Mmoja (1) wa Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika dhidi ya Rushwa (AUABC);

2. **LINAMCHAGUA NA KUMTEUA** afuataye kama Mjumbe wa AUABC kwa muhula wa miaka sita (6):

| NA | JINA | JINSIA | NCHI | UKANDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Nadia Annouz | Mwanamke | Morocco | Kusini |

**UAMUZI KUHUSU UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA UMOJA WA AFRIKA YA WAKAGUZI WA NJE (BoEAs) – Doc. EX.CL/1546(XLV)**

**Baraza Kuu,**

1. **LINAZINGATIA** mapendekezo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 ya Kanuni za Fedha za Umoja wa Afrika, yaliyowasilishwa na Wakuu wa Kanda kufuatia mashauriano ndani ya kanda husika;

2. **LINAAMUA** kuwateua, pamoja na wajumbe wa daraja la kwanza, Mkuu wa Taasisi za Juu za Ukaguzi kama wajumbe wa Bodi ya Wakaguzi wa Nje wa Umoja wa Afrika (BoEA) kufanya kazi za ukaguzi kwa miaka ya fedha 2024 na 2025 kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Sheria za Fedha za Umoja wa Afrika.

| **UKANDA** | **MWAKILISHI** |
|---|---|
| UKANDA WA KATI | EQUATORIAL GUINEA |
| UKANDA WA MASHARIKI | JAMHURI YA MAURITIUS |
| UKANDA WA KUSINI | UFALME WA ESWATINI |
| UKANDA WA MAGHARIBI | JAMHURI YA COTE D’IVOIRE |

# UAMUZI KUHUSU MAOMBI YA KUGOMBEA YA AFRIKA KATIKA MFUMO WA KIMATAIFA

**Baraza Kuu;**

1. **LINAZINGATIA** Ripoti ya Kamati ya Mawaziri kuhusu Maombi ya kugombea ya Afrika katika Mfumo wa Kimataifa;

2. **ZAIDI LINAZINGATIA** maamuzi ya Baraza yakiomba Jamhuri ya Ghana, Jamhuri ya Gambia na Ufalme wa Lesotho kushauriana na kukubaliana kuhusu mgombea mmoja Mwafrika wa Nafasi ya **Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola** wakati wa uchaguzi uliopangwa kufanyika Oktoba 2024;

3. **LINAPONGEZA** kujiondoa kwa **Jamhuri ya Muungano ya Tanzania** (Ukanda wa Afrika Mashariki) kwa kuzingatia ari ya mshikamano wa Afrika na maadili ya mgombea wake wa Nafasi ya **Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola**;

4. **LINAREJEA** uidhinishaji wa mapema uliofanywa na Mkutano wa Kawaida wa 44 wa Baraza Kuu wa **Dkt. Khaled El-Anany** wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika) kuwa mgombea wa Afrika wa nafasi ya **Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kipindi cha 2025-2029** kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika katika robo ya mwisho ya 2025, mjini Paris, Ufaransa;

5. **PIA LINAREJEA** Uamuzi wa Mkutano wa 44 wa Baraza Kuu wa Februari 2024 ulioidhinisha mgombea wa Zambia kwa Nafasi ya Rais na mgombea wa Morocco kwa Nafasi ya Makamu wa Rais wa INTERPOL; na **LINAOMBA** mashauriano zaidi na Nchi Wanachama zinazoshindana kwa ajili ya nafasi hizi kwa kuzingatia kanuni elekezi za msingi za umoja wa Afrika, mshikamano na maridhiano;

6. **LINAREJEA ZAIDI** uidhinishaji wa mgombea wa Senegal kwa Nafasi ya Mkurugenzi wa Kanda wa WHO kwa Afrika na pia **LINAOMBA** mashauriano zaidi na Nchi Wanachama ambazo ziliwasilisha wagombea kwa nafasi hii;

7. **LINASISITIZA** uidhinishaji wa mapema wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Ukanda wa Afrika ya Kati) na Jamhuri ya Liberia (Ukanda wa Afrika Magharibi) kwa Viti Visivyo vya Kudumu kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2026-2027; pamoja na Jamhuri ya Zimbabwe kwa kipindi cha 2027-2028;

8. **LINAVIOMBA** Vikundi vya Afrika kufuatilia utekelezaji wa Maamuzi haya na kutoa msaada unaohitajika wa kisiasa na kiufundi;

9. **LINAREJEA** Uamuzi wa Mkutano wa 44 wa Baraza Kuu la Februari 2024 kwamba Ukanda wa Kusini mwa Afrika inapaswa kutoa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa Mkutano wa 84 kwa nia ya usawa wa kikanda. **ZAIDI LINAAMUA** kwamba maombi ya Jamhuri ya Burundi kugombea Nafasi ya Rais wa Mkutano wa 84 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) kwa kipindi cha 2029-2030, kwenye uchaguzi utakaofanyika Juni 2028, New York, Marekani, hayatazingatiwa kwa kuzingatia mbinu ya zamu iliyopitishwa na Baraza Kuu mnamo Februari 2024.

10. **LINAIDHINISHA MAOMBI YAFUATAYO YA SERIKALI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Uongozi la *Wakala wa Kimataifa wa Nishati ya Atomiki (IAEA) kwa kipindi cha 2024 -2026***, *kwa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2024 huko Vienna, Austria, maombi ya:*

- **Ufalme wa Moroko** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**B.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya a **Mjumbe wa Tume ya Sheria ya Biashara ya Kimataifa kwa kipindi cha 2025-2028,** kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2024, huko New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Burundi** (Ukanda wa Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Kongo** (Ukanda wa Afrika ya Kati)
- **Jamhuri ya Côte d'Ivoire** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Ghana** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Sierra Leone** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Zambia** (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)
- **Inasubiri** (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)
- **Inasubiri** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**C.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya a **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2025-2027**, kwa uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2024 huko New York, Marekani, maombi ya :

- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** (Ukanda wa Afrika ya Kati)
- **Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia** (Ukanda wa Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Kenya** (Ukanda wa Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Benin** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Gambia** (Ukanda wa Afrika Magharibi)

**NB:** ***Viti vitano tu (05) ndivyo vinapatikana kwa Afrika*.**

**D.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Idadi ya Watu kwa kipindi cha 2025-2027,** kwa uchaguzi uliopangwa tarehe 23-24 Julai 2024, mjini New York, USA, maombi ya :

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**11. LINAZINGATIA MAOMBI MAPYA YA SERIKALI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA :**

**A.** Kwa ajili ya kuwa mwenyeji **wa Ofisi ya Ukanda wa Afrika ya Mkutano wa Hague kuhusu Sheria ya Kimataifa ya Binafsi kwa kipindi cha 2025-2027**, kwa uchaguzi utakaofanyika Machi 2025 huko New York, Marekani, maombi ya :

- **Ufalme wa Moroko** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**B.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO) kwa kipindi cha 2026-2027**, kwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2025, London, Uingereza, maombi ya:

- **Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia** (Ukanda wa Afrika Mashariki)

**C.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi *na Baraza la Uendeshaji Posta la Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kipindi cha 2025-2027***, *kwa uchaguzi utakaofanyika Septemba 2025 huko Dubai, UAE, maombi ya:*

- **Ufalme wa Moroko** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**D.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi Tendaji ya UNESCO kwa kipindi cha 2025-2029**, kwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2025 huko Samarkand, Uzbekistan, maombi ya:

- **Ufalme wa Moroko** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)
- **Jamhuri ya Togo** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Ukanda wa Afrika Kaskazini)
- **Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia** (Ukanda wa Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria** (Ukanda wa Afrika Kaskazini)

**E.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Bodi Tendaji ya UNESCO kwa kipindi cha 2027-2031**, kwa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2026 huko Paris, Ufaransa, maombi ya:

- **Jamhuri ya Senegal** (Ukanda wa Afrika Magharibi)

**F.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mwanachama asiye wa Kudumu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) kwa kipindi cha 2029**, kwa uchaguzi utakaofanyika Juni 2028, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho ya Nigeria** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Jamhuri ya Guinea Bissau** (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Ufalme wa Moroko** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)
- **Libya** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**NB:** ***Viti viwili (2) vimetengwa kwa ajili ya Afrika. Kundi la Kiafrika huko New York linaombwa kushauri Kanda zote mbili kushauriana na kukubaliana juu ya mgombea mmoja kwa kila Kanda.***

**G.** Kwa uchaguzi wa Nafasi ya **Mwanachama asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2029-2030,** kwa uchaguzi utakaofanyika Juni 2028, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Uganda** (Ukanda wa Afrika Mashariki)

**H.** Kwa ajili ya uchaguzi kwa Nafasi ya **Mwanachama asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2031-2032,** kitakachofanyika Juni 2030, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)

**I.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mwanachama asiye wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kipindi cha 2032-2033**, utakaofanyika Juni 2031, New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**J.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 2026-2028**, kwa uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2025 huko New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Kiarabu ya Misri** (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)
- **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** (Ukanda wa Afrika Mashariki)
- **Jamhuri ya Afrika Kusini** (Ukanda wa Kusini mwa Afrika) *Kuchaguliwa tena*
- **Jamhuri ya Mauritius** (Ukanda wa Afrika Mashariki)

**K.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Baraza la Haki za Binadamu kwa kipindi cha 202 7-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2026 mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria** (Ukanda wa Afrika Magharibi)

12. **LINAIDHINISHA MAOMBI MAPYA YA WATU BINAFSI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola** kwa kipindi cha 2024-2029**,** wakati wa uchaguzi uliopangwa kufanyika Oktoba 2024, mjini London, Uingereza, maombi ya:

- **Mhe. Shirley Ayokor Botchwey** wa Jamhuri ya Ghana (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Mhe. Dkt. Mamadou Tangara**, Waziri wa Sasa wa Mambo ya Nje wa Gambia (Ukanda wa Afrika Magharibi)
- **Seneta Joshua Phoho Setipa**, wa Ufalme wa Lesotho (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)

**B.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Posta wa Kimajumui (PAPU) kwa kipindi cha 2025-2029**, uliopangwa kufanyika Oktoba 2024 mjini Arusha, Tanzania, maombi ya:

- **Bi. Jessica Hope SSENGOOBA** wa Jamhuri ya Uganda (Ukanda wa Afrika Mashariki) ***Kuchaguliwa tena***

**C.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha 2025-2027**, uliopangwa kufanyika Oktoba 2024 huko New York, Marekani, maombi ya:

- **Profesa Frans Jacobus Viljoen** wa Jamhuri ya Afrika Kusini (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)
- **Mheshimiwa Jaji Edward Amoako ASANTE** wa Jamhuri ya Ghana (Ukanda wa Afrika Magharibi)

**D.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kitengo cha Ukaguzi wa Pamoja (JIU)** kwa kipindi cha 2025-2030, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Novemba 2024, New York, Marekani, maombi ya:

- **Bw. Makiesse Kinkela Augusto** wa Jamhuri ya Angola (Ukanda wa Kusini mwa Afrika)
- **Bw. Tesfa Alem Seyoum** wa Nchi ya Eritrea (Ukanda wa Afrika Mashariki)
- **Bw. Robert Nguei Mule** wa Jamhuri ya Kenya (Ukanda wa Afrika Mashariki)

**E.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Codex Alimentarius** kwa kipindi cha 2025-2027, uliopangwa kufanyika Novemba 2024 mjini Geneva, Uswizi, maombi ya:

- **Dkt. Allan Azegele** wa Jamhuri ya Kenya (Ukanda wa Afrika Mashariki)

**F.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Utumishi wa Umma wa Kimataifa (ICSC) kwa kipindi cha 2025-2027**, wakati wa uchaguzi utakaofanyika Novemba 2024 mjini New York, maombi ya:

- **Bw. Larbi DJACTA** wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika) ***Kuchaguliwa tena***
- **Bw. Elhassane ZAHID** wa Ufalme wa Morocco (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**13. LINAZINGATIA MAOMBI MAPYA YA WATU BINAFSI YALIYOWASILISHWA NA NCHI WANACHAMA:**

**A.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mjumbe wa Kamati dhidi ya Mateso (CAT)**, **kwa kipindi cha 2026-2029**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2025, mjini Geneva, Uswisi, maombi ya:

- **Bw. Abderrazak Rouwane** wa Ufalme wa Morocco (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)

**B.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria ya Bahari (ITLOS) kwa kipindi cha 2026-2035**, uliopangwa kufanyika Juni 2025 mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Dkt. Sylvia Adusu** wa Jamhuri ya Ghana (Ukanda wa Afrika Magharibi)

**C.** Kwa ajili ya uchaguzi wa Nafasi ya **Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya Utumishi wa Umma wa Kimataifa (ICSC) wa Kimataifa kwa kipindi cha 2026-2030**, kwa ajili ya uchaguzi utakaofanyika Juni 2025, mjini New York, Marekani, maombi ya:

- **Bw. Ali Ayad Ali Kurer** wa Nchi ya Libya (Ukanda wa Kaskazini mwa Afrika)
- **Balozi Andrew Gbebay Bangali** wa Jamhuri ya Sierra Leone (Ukanda wa Afrika Magharibi)

**NB:** ***Kiti kimoja (1) kimetengwa kwa ajili ya Afrika. Kundi la Kiafrika huko New York linaombwa kuwezesha mashauriano kati ya Kanda zote mbili na kukubaliana juu ya mgombea mmoja wa nafasi hii.***

**14. KUHUSU MASUALA MENGINE**

**Baraza;**

A. **LINAPONGEZA** kazi ya Kamati ya Mawaziri kuhusu Maombi ya kugombea ya Afrika katika Mfumo wa Kimataifa na Sekretarieti yake chini ya uongozi wa Kamishna wa Masuala ya Siasa, Amani na Usalama;

B. **LINATOA WITO KWA** Nchi Wanachama wa AU kuendelea kutoa msaada wa kisiasa unaohitajika kwa Kamati kwa kuzingatia moja ya thamani kubwa ya mshikamano wa Kiafrika kwa lengo la jumla la kuhakikisha uwepo thabiti wa Waafrika katika Mfumo wa Kimataifa;

C. **LINAELEZEA** wasiwasi wake kuhusu muda wa vikao vya Kamati sambamba na Vikao vya Baraza Kuu, na **LINAAMUA** kuwa kikao hicho kitafanyika siku moja kabla ya kufunguliwa kwa Vikao vya Baraza Kuu;

D. **LINAIOMBA** Kamisheni kuendelea na mpango wa *E-Portal* kwa ajili ya kuwasilisha maombi mtandaoni na kuandaa mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya programu za maelekezo zinazoendelea kwa Nchi Wanachama wa AU;

E. **LINAZINGATIA** kutofuatwa kwa Kanuni ya Utaratibu ya Kamati ya Mawaziri kunakofanywa na Nchi Wanachama na **LINAOMBA** kuwepo matumizi ya utaratibu wa vikwazo kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizo za Utaratibu;

F. **ZAIDI LINAIOMBA** Kamisheni kuandaa kikao maalum cha Kamati ya Mawaziri mjini New York mnamo Septemba 2024 kando ya Mkutano wa 79 wa UNGA, na Kikao Kazi cha Mawaziri kwa wakati ufaao. Mkutano utashughulikia masuala ambayo hayajakamilika kuhusiana na mbinu za kazi na matumizi ya Kanuni za Utaratibu za Kamati ya Mawaziri; na

G. **LINAIAGIZA** Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), kupitia kamati zake ndogo husika, kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za Kamati ya Mawaziri kuhusu Maombi ya Kugombea ya Afrika ndani ya Mfumo wa Kimataifa kutoka Bajeti ya Nchi Wanachama.